NDOA NI MFULULIZO WA HUDUMA

# MAHITAJI YA KIPEKEE

## KITABU CHA KUJIFUNZIA

### JUZUU 3

Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, mkiwafundisha kushika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari. Amina. (Mathayo 28: 19-20)

FDM .WORLD

Craig Caster

*Unique Needs* in Swahili
Marriage Is a Ministry series, Volume 3 of 5

***Mahitaji ya kipekee*** **ni juzuu ya 3** katika Kitabu cha Ndoa ni Mfululizo wa Huduma

**Juzuu nyingine katika Kitabu cha Ndoa ni Mfululizo wa Huduma**

*Msingi Imara* (juzuu ya 1)
*Upendo ni Nini* (juzuu ya 2)
*Utimilifu wa Kimwili* (juzuu ya 4)
*Uongozi wa Kimungu* (juzuu ya 5)
Mwongozo wa Kiongozi

**Vitabu vingine vya Kujifunzia kutoka FDM.world**

*Msingi wa Kweli kwa Kikristo: Msingi Imara kwa Mwanafunzi* na Craig Caster
*Malezi ni Mfululizo wa Huduma* na Craig Caster
*Kuwaelewa Vijana* na Craig Caster

Vitabu vyote vya kujifunzia kutoka FDM.world vinapendekezwa kwa matumizi ya masomo binafsi, katika vikundi vidogo vidogo kama nyenzo za kujifunzi na kutolea ushauri na saha.

Tafadhali kumbuka: Kurasa zote tupu kwenye nakala halisi zimeondolewa. Kwa sababu hiyo, baadhi ya namba za kurasa zinaweza kurukwa.

# Mahitaji ya Kipekee

Ndoa ni Mfululizo wa Huduma

Juzuu 3

Craig Caster

Basi, enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote hata ukamilifu wa Dahari. Amina (Mathayo 28:19-20)

FAMILY
DSCP FSHP
MINISTRIES
Simu: (619) 590-1901
Barua pepe: info@FDM.world
Wavuti: www.FDM.world

*Mahitaji ya Kipekee* , Kitabu cha Ndoa ni Mfululizo wa  Huduma, Juzuu ya 3, na Craig Caster
ISBN 978-1-7331045-2-4
© 2019 Google Sheria na Masharti ya Tovuti Faraghani
Waendelezaji Wasanii Kuhusu Google Haki zote zimehifadhiwa.
Marekebisho ya 09012020.

Isipokuwa itakaporekebishwa vinginevyo, lakini kwa sasa nukuu zote za Maandiko zimetolewa katika Biblia ya Swahili Union Version (SUV). Hatimiliki © Chama cha Biblia cha Tanzania na Chama cha Biblia cha Kenya (1997), Maandiko yote yametumika kwa ruhusa maalumu na haki zote zimehifadhiwa.

Pasipo ukomo wowote, si ruhusa kunakili, kuchapa au kuandika upya chapisho au sehemu ya chapisho (kwa mfumo wa e-book) au namna nyingine yoyote inayoweza kutengenezwa, kutunzwa; kwa umbo au kwa namna yoyote ile (kielektroniki, mekanikia, fotokopi, kurekodi au vinginevyo); bila ruhusa toka katika hatimiliki zilizotajwa hapo juu.

YALIYOMO

Dibaji……………………………………………………………………………………………………….vi

Utangulizi ..........................................................................................ix

Somo la 1: Mahitaji ya Ushirika wa Kibiblia ……………………………………………..1

Somo la 2: Mahitaji ya Wanaume. ...................................................……9

Somo la 3: Jihadharini na Ushawishi wa Kidunia……….........................……17

Somo la 4: Mke anayethibitisha Mamlaka……………………………………………23

Somo la 5: Matendo ya Kawaida yasiyothibitisha Mamlaka.......................31

Somo la 6: Mahitaji ya Wanawake ...................................................…37

Somo la 7: Zawadi kutoka kwa Mungu. .........................................……45

Somo la 8: Kumthamini Mkeo ...................................................................53

Somo la 9: Uongozi wa Familia ni Kazi ya Mwanaume……………………………59

Somo la 10: Uongozi Mzuri Haubadiliki ……...............................................65

Rasilimali Viambatisho ............................................. ................................69

Maelezo ya mwisho ........................................................................131

Kuhusu Mwandishi ........................................................................133

Kuhusu  Huduma ya Uanafunzi katika Familia ..............................……135

## Dibaji

Mungu aliumba taasisi tunayoiita ndoa, na leo iko chini ya shambulio kali. Kauli hiyo inaweza kusikika kama ya kushangaza kwako, lakini kuna athari mbaya zaidi ambayo hutoka ndani ya uhusiano kati ya mume na mke. Baada ya wanandoa kuoana, kila mmoja huanza kuvuta kwake kulingana na mahitaji na matakwa yake. Kadri muda unavyopita, shida hazijasuluhishwa, kuvunjika moyo, kuchanganyikiwa na hasira huweza kuleta uchungu ambao husababisha chuki na kulipiza kisasi. Ikiwa watu wawili huingia katika ndoa wakiwa na matarajio makubwa kama haya na nia njema, kwa nini sasa ndoa nyingi hushindwa? Kwa maana nyingine, nini wanandoa wengi wanasuluhisha uhusiano ambao haujatimilika?

Kitabu hiki kimetolewa wakfu kwa Mungu kwa sababu ya shauku yake kwa kila mwanandoa kupata baraka alizokusudia katika ndoa. Wakati watu wawili wanapoungana kama mume na mke bila mafunzo juu ya kanuni za Mungu na mara nyingi bila mifano ya kimungu kutoka kwenye maisha yao ya nyuma, hawa hujikuta hawajui kabisa jinsi ya kutendeana. Wanaweza kuleta machungu ya zamani, kutengwa na waliowapenda pamoja na hisia hasi ambazo huongeza changamoto. Kupitia kitabu hiki, Mungu atafunua ukweli usiopingika ambao unapaswa kufuatwa, la sivyo matokeo yatakuwa ya kukatisha tamaa na kutokufurahisha; kwa kifupi, ni maumivu makubwa.

Takwimu zinaonyesha kuwa ndoa nyingi kati ya Wakristo huishia kwenye talaka. Kama watoto wa Mungu na warithi wa ahadi zake zote, kwa nini waamini wanashindwa? Shida ni ukosefu wa maarifa na mafunzo juu ya kanuni za kibiblia. Kwa kusikitisha, kwa sasa Kanisa haliweki juhudi za kutosha katika eneo hili ili kugeuza wimbi ambalo linasomba watu wengi chini ya njia ya uharibifu. Wanandoa wanahitaji sana mafundisho ya kibiblia, wakifundishwa na wengine katika ukweli wa Mungu. Waamini wanapojifunza kile ambacho Mungu anataka na kuamua kumfuata kama wanafunzi wa Kristo, watapokea neema na nguvu ya kushinda shida yoyote.

Mungu anataka kujionyesha mwenye nguvu kwa niaba yetu na anataka tumtukuze katika ndoa zetu; lakini lazima tumkubali pia. Tunajua ndoa ni muhimu kwa Mungu, lakini Wakristo wengi hata baada ya miaka kumi ya ndoa bado wanahisi kutostahili kuwafundisha wengine. Fikiria mtu ambaye amekuwa akifanya kazi fulani kwa miaka kumi; si angeweza kujisikia fahari *sana* kumfundisha mtu mwingine. Na Mungu anajali zaidi juu ya jinsi tunavyowatunza wenzi wetu kuliko miito yetu.

Unapokamilisha mfululizo huu wa mafunzo kwa maombi, Mungu atafunua kusudi lake kwako kama mume na mke. Maarifa yote yatategemea ukweli wa kibiblia tu. Vitabu hivi vya kujifunzia vitakuongoza kwa kutumia Maandiko na kukupa vielelezo vya vitendo ili kukusaidia kutekeleza kanuni unazojifunza. Mfululizo huu pia unakusudiwa kuwa zana ya kuwafundisha wengine. Wakati macho yako yatakapofunguliwa kwa njia ya ajabu amabyo Mungu hutumia kuyabadilisha maisha yako, utaona kwamba wengine wengi wanahitaji msaada pia.

*Bwana Mungu, asante kwa kufunua moyo na mapenzi yako kwetu katika Neno lako. Tafadhali wabariki wale wanaopitia kitabu hiki. Fanya kanuni ziwe wazi. Wape mioyo ya uyenyekevu kuwasamehe wale ambao wamewaumiza na shauku ya kuomba msamaha kutoka kwa wale ambao wamewaumiza. Mungu, utukuzwe ndani na kupitia ndoa za wale ambao wako tayari kukufuata. Amina.*

## Utangulizi

Kitabu hiki kimeandaliwa kukuleta kwenye njia ya uanafunzi, ambayo inamaanisha kutembea katika kanuni za Mungu. Tunapotumia maneno kama *kutembea*, tunatumai unaelewa kuwa kuishi chini ya kanuni hizi ni jambo la msingi kama vile kujifunza kutembea.

Malengo ya kitabu chetu ni:

1. kukuonyesha kuwa Mungu hutoa kanuni za ndoa,
2. kukuwezesha kupata mbinu na matumizi ya kanuni hizi, na
3. kuongoza ndoa yako na familia yako katika msamaha, uponyaji na umoja unaokuja kwa kumtii Mungu.

Huduma za Uanafunzi katika Familia zipo ili kusaidia kuelimisha kuhusu mwili wa Kristo katika maeneo muhimu. Kukosa kuwafundisha wengine, kwa leo kunahusiana moja kwa moja na kiwango cha kutofaulu katika ndoa. Na tunalijuaje hili? Tunajua kwa njia ya kuona, uzoefu na hupatikana katika takwimu zilizothibitishwa wakati huu.

### Mchakato

Masomo yamegawanywa katika juzuu tano. Anza na juzuu ya 1 na endelea kupitia kila juzuu kwa mpangilio. Kurukia juzuu au sehemu ambayo inachochea shauku yako inashawishi ingawa haishauriwi; kwa sababu kuna mwendelezo katika kila juzuu na kila somo. Kwa mfano, unaweza kutaka kujua mahitaji ya urafiki wa mwanaume au mwanamke, lakini kuna kanuni za kibiblia ambazo lazima ujifunze kabla ya kuzingatia mahitaji ya mme/mke wako kwa njia ya kimungu. Jitahidi kumaliza somo moja kila siku kwa siku tano. Kujijengea tabia ya kusomo kila siku bila kukosa ni ufunguo wa mafanikio ya kiroho.

Kanuni hizi zimejaribiwa na kuthibitika kufanikiwa. Nimeyashuhudia katika ndoa yangu mwenyewe na kupitia maisha ya watu, hata katika masomo ya ushauri na ndoa. Tafadhali elewa, huu *sio* mwongozo wa "Hatua tano Rahisi za Ndoa". Ufuasi wa kibiblia ni kazi ngumu na inakuhitaji ujikabidhi kwenye mapenzi ya Mungu unapobadilisha mitazamo na tabia zako. Mchakato utahitaji kujituma, kujitolea na unyenyekevu.

### Kuianza Kila Siku

- Ona kila somo la kila siku kuwa kama wakati mzuri unaotumia na Mungu wako na mtarajie yeye azungumze nawe kupitia Neno lake.

- Anza kila siku kwa maombi, ukimwomba Mungu akufunulie ni wapi unahitaji kubadilika na kukupa uwezo wa kutumia kile unachojifunza.

- Kuwa na fikra za kutafakari. Usikimbilie kusoma tu ili kusema kwamba umemaliza. Mpe Mungu wakati wa kusema nawe na tafakari juu ya yale unayojifunza.

**Mambo ya Kuzingatia**

- Mafunzo haya ni kipaumbele kipya hivyo utahitaji muda wa kujitolea. Masomo yanapaswa kufanywa kila siku. Ukikosa siku, *usiiruke* , bali fanya kazi kumaliza masomo yote kwa utaratibu.
- Maandiko yanasema wazi kwamba ndoa ni muhimu kwa Mungu. Ikiwa unajitahidi kumaliza masomo, omba juu ya vipaumbele vyako na ahadi nyingine. Pata msaada wa mshirika uwayejituma katik sala ikiwa ni lazima.
- Kumbuka, mme/mke wako ni mwenzi muhimu katika juhudi hii. Soma pamoja naye au kando yake, lakini kila wakati jadili kile ulichojifunza na jiombee ili uweze kutekeleza mabadiliko yoyote yanayohitajika.
- Masomo yanaweza kutofautiana katika idadi ya maarifa yanayowasilishwa. Baada ya kumaliza kila moja, tazama mbele kwa somo linalofuata na kupanga muda wako na Mungu na kufaidika zaidi.
- Nafasi imetolewa kwa kujibu maswali na kurekodi mawazo yako na sala. Ikiwa umepakua na kuchapisha kitabu hiki cha kujifunzia, tunashauri uweke kwenye mfumo wa kitabu chenye sehemu tatu na ujumuishe karatasi ya ziada ya uandishi binafsi na notsi .

**CHIMBA ZAIDI**

Sehemu hii inaashiria fursa ya kusoma Maandiko na kuyahusisha na mada inayowasilishwa. Utaijua zaidi Biblia, kanuni za kibiblia za ndoa, na kile ambacho Mungu anatarajia kutoka kwako kama mme/mke.

**FAILI LENYE UKWELI**

Sanduku kama hili hutoa ufafanuzi wa maneno au vifungu kutoka kwenye Biblia. Tumechukua tahadhari kubwa kutumia faharasa za Biblia zinazojulikana, zenye sauti za kimantiki na ufafanuzi kwa ufafanuzi, unaorejelewa Maandiko. Nyingi ya fasili hizi zinaonekana katika,*Kiambatisho R: Faharasa*

**Kujichunguza**

Unapojifunza kanuni za kibiblia, sehemu hii hutoa wakati wa kujichunguza, kutafuta maeneo ambayo uboreshaji wa kibinafsi unahitajika. Nafasi hutolewa kwa ajili ya kuorodhesha ufahamu, maungamo, na maombi ya nguvu na hekima ya kufanya mabadiliko hayo. Kipengele kimojawapo katika mchakato wa uanafunzi ni uwajibikaji binafsi. Ikiwa Mungu amekufunulia kuwa umemkosea mwenza au mtoto wako, basi ungama dhambi yako kwao na uombe msamaha. Jizoeze kufanya hivyo mara kwa mara hata kama utafanya pasipo kujulikana kwa yeyote.

***MPANGO KAZI***

Baada ya kusoma kanuni za kibiblia, sehemu hii inakupa changamoto ya kuchukua hatua na kutumia kile ulichojifunza katika ndoa yako. Ili kuwa wanafunzi wa kweli lazima tuelewe kwamba Mungu hatamani tu tuweze kukua katika maarifa, lakini pia anahitaji tuyaishi.

**Rasilimali Viambatisho**

Tafadhali tumia viambatisho mwisho wa kitabu hiki cha kujifunzia. Vipo kwa ajili ya ukuaji wako na tunavirejelea katika kitabu hiki cha kujifunzia. Kabla ya kuanza safari hii nzuri, tafadhali jaza *Kiambatisho A: Barua ya Kujitolea* (juzuu 1).

**Mwongozo wa Kiongozi**

Mwongozo wa kiongozi unapatikana kwenye *FDM.world under free Ministry downloads*. Vifaa vyote kwenye wavuti yetu hujikita katika uanafunzi na hutolewa bure.

## Somo 1

## Mahitaji ya Ushirika wa Kibiblia

Kila juzuu katika safu hii ya Ndoa ni Mfululizo wa Huduma hujengwa juu ya juzuu iliyopita, na juzuu hii pia sio ya kuacha. Hakikisha unasoma kila moja kwa mpangilio *ili* uweze kufahamu dhana zilizotangulia kabla ya kuchimba katika kitabu hiki.

Tunaanza somo hili kwa mahitaji ya ushirika ya mwanaume, au mume, na kisha tuendelee kujua kile ambacho mwanamke anahitaji. Tunapaswa kuwa tayari na uzoefu na neno *huduma* na jinsi inavyotumika kwa ndoa zetu. Kumbuka, tunapaswa kuwa wahudumu katika nyumba zetu, tukiwahudumia waume/wake zetu kama Kristo alivyofanya na bado anaendelea kutuhudumia. Jukumu lililotolewa na Mungu katika kukidhi mahitaji ya urafiki wa mwenza wako ni huduma inayokusudiwa kuwakilisha upendo na kumtukuza Mungu.

Unapojifunza kutumia ukweli wa Mungu maishani mwako, mabadiliko yatatokea katika mawazo na tabia yako. Huu ni muujiza wa kutii Neno la Mungu, ambao sio rahisi kila wakati kuutimiza, lakini wakati wote huzaa matunda ya haki. Utii huu *lazima* utangulie mabadiliko. Mtajikuta mnakidhi mahitaji ya kina ya kila mmoja, ambayo huleta utimilifu zaidi. Na tunapotaja Neno la Mungu, amini kwa moyo wako wote kwamba huu ndio msingi pekee wa kujenga na kudumisha msingi wako imara — uhusiano binafsi na Yesu Kristo. Ni mahali pekee ambapo tunaweza kupokea baraka na nguvu za Mungu kutuwezesha kutimiza mapenzi na kusudi lake.

Tayari tumejifunza juu ya mahitaji ya ushirika amabayo ni ya kawaida kwa mume na mke, yaani hitaji letu kuu, ambalo ni upendo. Kumbuka daima akilini mwako juu ya 1 Wakorintho 13 na vidokezo vyote vinaelezea njia ambayo Mungu anataka tupendane. Rejea kifungu hiki mara nyingi unapotafuta kujenga upendo usio na masharti kati yako na mwenzi wako.

Jambo la kuzingatia kwa waume: Kama kiongozi wa nyumba yako na kwa jukumu la kumpenda mkeo kama vile Kristo anavyolipenda Kanisa, jifunze zaidi 1 Wakorintho 13. Unamwakilisha Mungu na ukweli wake kwa mke na watoto wako.

### Mahitaji ya Ushirika Yamewekwa na Mungu

Waume na wake wana mahitaji ya ushirika ambayo ni ya kipekee kwa kila mmoja, kama watu wa kiume na wa kike. Mahitaji haya ni ya ulimwengu wote, yamewekwa ndani yetu na Mungu na Biblia ndio chanzo pekee sahihi cha maarifa juu ya kuhudumiana kwa kusudi la kuyatimiza. Tunaanza kujifunza katika Waefeso 5: 22-23 na mahitaji ambayo ni maalum kwa wanaume. Kwa nini wanaume kwanza? Kwa sababu tu Maandiko yanafundisha kwa utaratibu huo, na maagizo kwa wanawake juu ya jinsi ya kukidhi mahitaji ya ushirika wa mwanaume.

Tunapojifunza matini hizi, fikiria kuwa Mungu aliumba umoja wa ndoa na kwa kufanya hivyo, alikuwa bado ana mpango na kusudi kwa wanaume na wanawake katika ndoa. Kinyume na maoni ya kawaida, ndoa haipo kutimiza matarajio yetu na matamanio yetu ya binafsi. Kwa mfano, wanandoa katika ushauri na saha kawaida huanza na orodha ya kile ambacho hawakipati katika uhusiano na namna ambavyo hali hiyo  kuwafanya wasiwe

furaha kabisa. Wengi wetu huanza bila kujua nini maana ya kupenda kwa njia ya Mungu. Ndoa ni kitu kizuri, kilichoundwa na Mungu kwa faida yetu na raha, lakini hii hufanyika tu tunapojitolea kutimiza mapenzi na makusudi yake.

Watu wengi hawajui ukweli huu wa msingi: Mungu ndiye mwanzilishi na mbunifu wa ndoa. Je! Unajua kuwa moja ya madhumuni makuu ya ndoa yako ni kumletea Mungu utukufu? Kutokuelewana juu ya kusudi la ndoa na ufafanuzi wa mapenzi ya kweli mara nyingi ni chanzo cha kutoridhika na kukatishwa tamaa, sababu wengi hawapati utimilifu wa baraka ambayo Mungu alitengeneza katika uhusiano huu. Nyingi ya shida hizi hutokana na kuwa na mtazamo wa ubinafsi. Lazima tufanye hivi kwa njia ya Mungu, la sivyo hatutatimilika, hili ni kwa wote.

**CHIMBA ZAIDI**

Kupitia uhusiano wako na Kristo, Mchungaji Mkuu, Mungu anaweza kufanya kazi ndani yako. Kazi hiyo ni nini na malengo ni yapi?

> Basi Mungu wa amani aliyemleta tena kutoka kwa wafu Mchungaji mkuu wa kondoo, kupitia damu ya agano la milele,yeye Bwana wetu Yesu awafanye ninyi kuwa wakamilifu katika kila tendo jema mpate kuyafanya mapenzi yake, naye akifanya ndani yetu lipendazalo mbele zake, kwa Yesu Kristo; Utukufu una yeye milele na milele.Amina(Waebrania 13: 20-21)

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

____________________________________________________________

Katika Yohana 17:17, Yesu anawaombea hawa wanafunzi wake, “uwaatakase kwa ile kweli yako. Neno lako ndio kweli. ” *Kutakasa* kunamaanisha "kufanya takatifu na kujitenga na dhambi," na kusababisha maisha ya kujitolea kwa Mungu. Maandiko haya yanaonyesha umuhimu wa Neno la Mungu katika kufanikisha chochote kulingana na mapenzi yake, au kama kiwango cha kutathmini lililo jema na baya, ambalo linajumuisha jinsi tunavyotenda ndani ya ndoa zetu.

**Kujichunguza 1**

Kama tulivyojifunza, mafanikio hutokana na kuwa na msingi imara, uhusiano wa kudumu na Yesu kupitia katika Neno la Mungu na maombi. Hii ndiyo njia pekee ya kujua mapenzi ya Mungu na kupokea nguvu na neema ya kufanikiwa katika huduma yetu ya ndoa. Kwa wakati huu, unawezaje kuelezea maisha yako ya kujitolea? Ikiwa haijawa sawa, ungama/tubu kwa Mungu na uweke mpango wa kuifanya iwe sawa.

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

Watu wako hapa duniani kutimiza mapenzi ya Mungu, ingawa wengine wanamkataa na wengine wanapokea zawadi yake ya wokovu katika Kristo Yesu. Na ndivyo ilivyo hata miongoni mwa waamini. Tunaweza kuchagua kufuata maagizo ya Mungu au kutotii. Lakini, ikiwa tunaelewa kuwa njia ya furaha na baraka hutoka kwake tu, basi haina maana kwamba katika maeneo yote ya maisha yetu tunahitaji kuwa tukimwangalia Bwana kwa kumuuliza, Unataka nifanye nini? Hivyo hatutakuwa tunakuwa tunafanya mapenzi yake kwa hiari yetu wenyewe. Mungu anatuahidi kutupa nguvu ya kufanikisha chochote kile. Petro wa pili 1: 4 inasema, "tumepewa ahadi kubwa na za thamani sana, ili kwa hizo mpate kushiriki katika tabia ya Kiungu, mkiepuka uharibifu uliopo duniani kwa tamaa." Haijalishi umekuwa mjinga au mbinafsi kiasi gani katika siku zako za nyuma, Mungu anaweza na atashinda yote. Wakati Biblia inaposema jambo nasi hatuamini, tunamwita Mungu mwongo.

Kama mume na mke, Mungu ana mpango na kusudi kwa kila mmoja wenu. Amekuita kwake mwenyewe, akubariki na ahadi zake na unapomtazama, kwa Neno lake, atakuongoza na kukupa nguvu. Nguvu ile ile iliyomfufua Yesu kutoka kwa wafu ina uwezo wa kukamilisha kila kitu ambacho Mungu anataka kwako.

> Na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio, jinsi ulivyo, kwa kadri ya utendaji wa nguvu za uweza wake, aliyotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho.(Waefeso 1: 19-20)

Hata wenzi wa kikristo huja kwenye ushauri na saha wakiwa hawana matumaini, wamejaa chuki. Hawatambui kwamba wameingia kwenye kujihurumia, hali ambayo ni kukataa nguvu za Mungu. Mungu hadanganyi watoto wake mwenyewe. Ametoa yote kwa ajili ya mafanikio yao "kama uweza wake wa kimungu ametupatia vitu vyote vinavyofungamana na uzima na kumcha Mungu, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu na fadhila" (2 Petro 1: 3); tatizo liko kwetu, mtazamo wa ubinafsi au ujinga kamwe haumtukuzi Mungu na hautoi ushindi kwake.

Wakristo wanashtuka kujua kwamba kiwango cha talaka kati ya waamini tangu 1997 kimefanana na ile ya wenzi wa ndoa walio nje ya imani. Lazima tupate ujasiri kwamba Mungu anaweza na atatupa maarifa na nguvu ya kufanikiwa katika ndoa. Mungu anataka kutukuzwa katika watoto wake. Aliunda umoja wa ndoa ili kujiletea utukufu. Ikiwa Mungu aliunda ndoa kama baraka kwa watoto wake na kumtukuza, ni nini kimeharibika?

**Urafiki Umefafanuliwa**

Ndani ya ndoa, watu wawili wanaungana kama marafiki. Hii inathibitisha maana na raha halisi inayowezekana ya kuwa katika umoja kama huo na mtu mwingine. Ukweli wa kushangaza, uliopotea kwa wengi, ni kwamba mafanikio yetu hayatoki ndani yetu. Utimilifu wa kweli huja tu kwa kujua na kufuata habari maalum ya Mungu juu ya jinsi ya kukidhi mahitaji ya ushirika wa kila mmoja, ambayo hupatikana tu katika Neno Lake.

**FAILI LENYE KWELI**

*Ushirika* –Mtu aliyeambatana nawe, au ni katika kampuni, kwa wao; mwenzi, rafiki, masilahi ya uhusiano maalum kama mwenzi, au rafiki.

**Kujichunguza2**

Eleza tathmini yako ya sasa juu ya taarifa zilizo hapo juu. Kuwa mwaminifu.

______________________________________________________________________

___________________________________________

______________________________________________________________________

___________________________________________

______________________________________________________________________

__________________________________________

______________________________________________________________________

___________________________________________

Mungu aliunda ndoa, ambayo ni ufunguo wa kutafuta na kufungua siri ya mapenzi. Kwa kuwa Biblia ni chanzo cha ukweli wa Mungu ulioandikwa, tunaiangalia yenyewe katika kile tunachotafuta, ambacho ni ufahamu wa kusudi la ndoa na jinsi ya kukidhi mahitaji ya kina kwa kila mmoja. Wakati wa kutafiti mafundisho juu ya somo fulani, ni muhimu kuanzia mwanzoni, ambapo ni Kitabu cha Mwanzo, kitabu cha kwanza cha Agano la Kale. Baada ya mwanadamu kuumbwa na Mungu na kupokea pumzi ya uhai (Mwanzo 2: 7), aliwekwa katika bustani ya Edeni kuitunza na kuiangalia (mstari wa 15). Mungu aliona vyote kuwa bora, kisha baada ya muda aliamua kwamba Adamu, kama alivyomtaja mtu wake, hakuwa na mshirika, msaidizi anayefanana naye, na hii haikuwa nzuri machoni pake. Mungu aliona yote mengine kuwa mazuri (Mwanzo 1: 4, 10, 12, 18, 21, 25), lakini hali ya Adamu *peke yake* haikuwa nzuri.

Mungu angeweza kuwaumba Adamu na Hawa kwa wakati mmoja, lakini alitaka Adamu atambue hitaji la mwenza na kusababisha baraka kubwa na amthamini mwanamke. Mithali 18:22 inasema,
"Apataye mke hupata kitu chema
naye ajipatia kibali kutoka kwa Bwana”

**FAILI LENYE UKWELI**
*Msaidizi- Ezer(*Kiebrania) ni mshirika, au mtu anayetoa msaada. Msaidizi wa Adamu Mwanzo 2:18 . Msaada wa Mungu kwa Waisraeli Hosea 13:9, Kutoka 18:4, Kumbukumbu 33:7, Zaburi 33:9;115:9-11

Bwana Mungu akasema, "Si vema mtu huyu awe peke yake…(Mw 2:18)

Mwandishi mmoja aliatoa ufafanuzi kuhusu kifungu hiki cha Kitabu cha Mwanzo kwa kusema;

> Utoaji wa Mungu wa kumpa Adamu mke ni mfano halisi wa kwamba Mungu hujua ni nini kinachomfaa mtu.
> Ushirika ulichukua nafasi ya mtu kuwa peke yake. Hata hivyo ili ushirika uwe wa kuridhisha, lazima kuwe na umoja katika ndoa (Mwanzo 1: 26-27; 2:18).

Wote wawili waume na wake wanahitaji kukumbatia mfano wa Mungu na umuhimu wa kukidhi mahitaji ya wenza. Hii ni hatua ya kwanza ya Mungu katika kuunda ndoa. Ikiwa Mungu ndiye muumba wako, je! Anakujua? Je! Anajua kilicho bora kwako?

Ni ujinga kuangalia ndani yetu ili kugundua kile tunachotaka na tunachohitaji ili kuweza kuridhika. Kwa asili tuna motisha binafsi na maarifa yetu mengi yametoka kwenye vyanzo vya ulimwengu ambavyo viko kinyume na Neno la Mungu. Lazima tuangalie Biblia kama chanzo chetu. Mungu ndiye muumbaji wetu na yeye peke yake ndiye anayeweza kuaminika kutuelezea mahitaji yetu ya kipekee ya ushirika na jinsi ya kuendana hayo.

**Mungu Anafafanua Mahitaji Yetu**

Kama tulivyojifunza kutoka katika Kitabu cha Mwanzo, wanaume na wanawake wameumbwa kama wenzi, lakini kila mmoja ana jukumu tofauti katika uhusiano wa ndoa. Ni Mungu tu ndiye anayeweza kutuambia kile alichotubunia sisi kutoa na kupokea kama waume au wake. Anajua pia kile tunachohitaji.

> Na Mungu wangu atawajazeni kile mnachohitaji kwa kadiri ya utajiri wake; katika utukufu ndani ya Kristo Yesu. (Wafilipi 4:19)
>
> Baba yenu anajua vitu mnavyohitaji kabla hamjamwomba. (Mathayo 6: 8)

Mungu anajua mahitaji yetu na hujitolea, lakini pia ametupa uhuru wa kuchagua haki au kinyume na mapenzi yake. Kwa kuzingatia ahadi zake, Je! Inaleta maana kukataa mpango wa Mungu na kushindwa kubariki na kubarikiwa ndani ya ndoa zetu?

Biblia inasema "Mungu ni upendo" (1 Yohana 4:16), na hii inamaanisha hasa kwamba Mungu anakupenda. Mungu anakupenda sana kiasi kwamba anataka mwenzi wako awe rafiki unayemhitaji. Mungu anampenda mwenzi wako sana kiasi kwamba anataka wewe uwe yule ambaye unahitajika. Mungu yuko tayari na anaweza kukugeuza kuwa mwenzi aliyekukusudia uwe.

Mungu anaweza kumuongoza mke kuwa mwenzi anayemtaka awe kwa mumewe, ili kukidhi nafsi ya kipekee na mahitaji yake. Mtu pekee anayeweza kuharibu hiyo ni mke, sio Mungu. Vivyo hivyo kwa mume. Mungu aliumba kila mmoja na kuweka mahitaji hayo ya kipekee ya urafiki ndani yao.

Mungu anasema, “Ninampenda mwenzi wako sana na ninataka kumimina neema yangu ndani yako, kukugeuza uwe mwanaume (au mwanamke) na mume (au mke) ninayetaka uwe, kutimiza mahitaji ya ushirika wa mwenzi wako. ” Na mtu pekee anayeweza kuharibu hiyo ni wewe. Je! Unaamini hivyo? Ikiwa sivyo, unachagua kuamini nini?

Lazima tujaribiwe kila wakati na kuchunguzwa katika mambo haya ya kiroho kwa sababu falsafa nyingi na nguvu hasi, za kipepo zinapingana na ukweli, ambao Mungu ameufafanua waziwazi. Tunaweza kupotoka kwenye shaka na kuogopa tunapoangalia kushindwa kwetu kutokana na mtazamo wa kiulimwengu ambao, sio mambo ambayo Mungu amekusudia kwetu.

> Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote,
> Wala usitegemee akili zako mwenyewe;
> Katika njia zako zote mkiri yeye,
> Naye ataonyesha mapito yako. (Mithali 3: 5-6)

Hii ni ahadi kutoka kwa Mungu Mwenyezi. Tunapoangalia kwenye Neno lake kwa mwongozo, tunaukaribia mwongozo huo kwa unyenyekevu, tukikubali kwamba Mungu anajua nia yetu ya asili katika kuelekea dhambi ya ubinafsi, lakini bado anatupenda. Ni kawaida kuwa na wasiwasi, kwa hivyo tukubali kwamba njia za Mungu sio njia zetu na tunathibitisha kwamba yeye peke yake ndiye hutoa ukweli tunaohitaji maishani.

> "Maana mawazo yangu si mawazo yenu,
> wala njia zenu si njia zangu," asema Bwana.
> "Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu
> sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu si juu
> sana kuliko njia zenu. Na mawazo yangu
> kuliko mawazo yako. ” (Isaya 55: 8–9)

Maandiko haya yanapaswa kuleta usadikishaji mkubwa. Hatuwezi kuamini njia zetu wenyewe na kile tunachofikiria au kuhisi juu ya uhusiano wetu wa ndoa au kile kilicho bora kwa mwenzi wetu. Ni kama Mungu amesimama upande mmoja wa kona na wewe upande mwingine. Mawazo yake yakiwa mbali sana na mawazo yako.

Kuna mgawanyiko kati ya ufahamu wa Mungu na ule wa mwanadamu juu ya ndoa. Kwa hivyo ni muhimu kupata hekima ya Mungu. Tunapaswa pia kukubali kwamba mioyo yetu ni yenye dhambi na tunahitaji Mungu atusafishe.

> Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote,
> Una ugonjwa wa kufisha;
> Ni nani anayeweza kuujua?
> Mimi, Bwana, nauchunguza moyo,
> Ninavijaribu viuno hata,
> Kumpa kila mtu kadiri ya njia zake;
> Kulingana na matunda ya matendo yake. (Yeremia 17: 9-10)

Hii inamaanisha hatuwezi kusema, "Sawa mpenzi, hiki ndicho ninachotaka unifanyie na kisha nitafurahi." Kwa maana hii ndiyo namna tunavyojidanganya. Wanandoa walikuja kwenye ushauri na saha na mke alikuwa na orodha ndefu ya matarajio yake kwa mumewe; huku akidhani atafurahi ikiwa atafanyiwa mambo yote hayo.

Yule mwanamke mwenye mtazamo alioamini ni nzuri hakuelewa mtazamo wa Neno la Mungu. Furaha yetu haitokani na wenzi wetu. Tumedanganywa ikiwa tunaamini hivyo na kamwe hatutapata furaha na utimilifu kwa njia hii. Njia pekee ya kuupata ni kwa kujikabidhi kwa Mungu na kufanya mapenzi ya Mungu kwa wenzi wetu. Hivyo ndivyo Mungu alivyoitengeneza ndoa.

Shida ya mke huyu ilikuwa kutokujua mapenzi ya Mungu katika uhusiano wa ndoa. Lakini Mungu hataki tuwe wajinga; ndiyo maana ametupa maarifa yote tunayohitaji katika Neno lake. Kwa bahati nzuri mwanamke huyo alichagua kupokea marekebisho ya Mungu.

Wanaume wengi hufanya makosa yanayofanana. Wao huweka matarajio binafsi juu ya wake zao, jambo ambalo hutoa matokeo yasiyotimizwa na kufanya wao kutenda kwa ghadhabu, kuogopa, kujitenga kwa hasira, au kujishughulisha na shughuli nyingine nje ya nyumba.

Wanaume, mtajifunza mahitaji yenu ya kipekee katika ushirika ni yapi, ni jinsi gani Mungu aliweka mahitaji haya ndani yenu, pamoja na jinsi mke wako anavyotimiza mahitaji hayo. Pia utajifunza jinsi ya kufanya kazi pamoja, sio kupima utendaji wa mke wako, lakini kuwa

mvumilivu, mwenye kusamehe na kutia moyo. Kumbuka kwamba wewe pia una jukumu la kukidhi mahitaji *yake ya* kipekee. Hii ni kama changamoto kwetu, yaani kazi fulani ngumu? Ni kweli, iko hivyo; lakini hii ndio tunayoiita hali ya "usawa kwa wote" .

**Kujichunguza 3**

Orodhesha matarajio uliyoweka kwa mwenzi wako, yapeleke mbele za Bwana, kiri tabia yoyote mbaya na andika maombi ya kujitolea kubadilika. Fikiria njia sahihi, za kimungu za kumruhusu mwenzi wako kujua nini ungependa kubadilisha.

____________________________________________________________________________

**CHIMBA ZAIDI**

Yesu anasema "ikiwa"anajitumia mwenyewe kama mfano. Katika Maandiko haya, tambua kinachokutaka ufanye na matokeo yake yatakuwa ni nini katika maisha yako.

> Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu, kama vile mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake.
>
> "Hayo niimewaambia, ili furaha yangu iwe ndani yenu, na furaha yenu ikamilike." (Yohana 15: 10–11)

____________________________________________________________________________

> Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu. Ombeni, nanyi mtapokea, ili furaha yenu itimizwe. (Yohana 16:24)

____________________________________________________________________________

Wanandoa wengi, hata baada ya kuwa pamoja miaka ishirini au zaidi, bado wanaishi kulingana na uelewa wao wenyewe, na Wakristo wakiwemo. Wanashangaa kwanini wanajisikia wapweke, kukata tamaa, au wana huzuni, hii ni kwa sababu ndoa zao

hazifanani na muundo wa Mungu. Katikati ya safari hii, wengi wanatengana kwa kufuata udanganyifu wa kawaida kwamba wanaweza kupata kile kinachowafanya wafurahi mahali pengine, wakichukua maoni yao yasiyokuwa na thamani. Wanaweza kukaa kwenye uhusiano mpya kutokana na kukosa malengo, kuchoka sana kujaribu, au kuingia kwenye njia ya uharibifu kwa "kuzama dhambini."

Tafsiri ya *The New Living* ya Kitabu cha Yeremia 17: 9 inasema moyo ni "mdanganyifu. . . na mwovu mno ”(NLT). Huwezi kwenda nje kutafuta kile unachotaka na kupata furaha ya kweli; badala yake utapata mambo yasiyo na faida. Waume na wake, lazima tumtazame Mungu, alituumba na kututengeneza ili tuwe katika uhusiano. Yeye ni mwaminifu na mwenye nguvu zote na yeye si mwongo.

Wakristo wajihadhari, kwa sababu hata Kanisa limeathirika na falsafa za ulimwengu, wakati mwingine hutegemea mafundisho ya ulimwengu na falsafa zake juu ya ndoa. Hata washauri "Wakristo" hutoa mwongozo ambao hautegemei Maandiko. Wakati Kanisa linapoacha kutumia Neno la Mungu lililoandikwa kama mwongozo wao, matokeo yake yatakuwa kutofaulu katika maisha ya watu wao.

Neno la Mungu linasema nini juu ya falsafa za kilimwengu?

> Angalieni mtu asiwafanye mateka kwa elimu yake ya bure na madanganyo matupu kwa jinsi ya  mapokeo ya wanadamu, kwa jinsi ya mafundisho wa awali ya ulimwengu, na sio kwa jinsi ya Kristo. (Wakolosai 2: 8)

________________________________________________________________
________________________________________________________________
________________________________________________________________
________________________________________________________________
_____________________________________________________

*Ufafanuzi wa Maarifa ya Bibilia hutoa maoni* mazuri juu ya andiko hili katika

Wakolosai:

> Falsafa ya uwongo huko Kolosai ilikuwa "mashimo" ( *ken ē s* , "tupu"), "udanganyifu," na msingi wa mila ya wanadamu. . . badala ya Kristo. Falsafa ya kweli ya Kikristo " iliteka kila fikira ili kumtii Kristo" (2 Kor. 10: 5). Falsafa ni upendo wa hekima, lakini ikiwa mtu anapenda hekima ambayo sio Kristo (Jumla ya hekima yote, Kol. 2: 3), anapenda sanamu tupu. Mtu kama huyo "atajifunza kila wakati lakini hataweza kuikubali kweli" (2 Tim. 3: 7). Aina hii ya falsafa inategemea kanuni za kimsingi za ulimwengu ( *stoicheia* , "kanuni za msingi" au "roho za kimsingi" [RSV]; rej. Kol. 2:20; Gal. 4: 3, 9). Hii inaweza kumaanisha roho waovu ambao huchochea uzushi kama huo na ambao Kristo alishinda juu yake (taz. 2 Kor. 4: 3-4; Efe. 6: 11-12). Falsafa kama hiyo ni ya kipepo na ya kidunia, sio ya kimungu au ya Kristo.
> waamini wasipokuwa  makini, falsafa kama hiyo inaweza kuwanasa, ikiwachukua "mateka." [3]

Unajisikiaje katika ndoa yako? Tupu, umekata tamaa, hauna matumaini? Andika mawazo yako.

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

_________________________________________________________________

Kwa ujumla kuna sababu mbili za kutofaulu. Labda unajua Neno la Mungu linasema nini na umeamua kutotii, au hujui Neno la Mungu na kwa hivyo unakosa baraka zake. Shida nyingi huibuka kwa sababu Wakristo hawajui Biblia inasema nini juu ya ndoa. Adui na ulimwengu wanaweza kuwashawishi kwa urahisi wale ambao wana msingi dhaifu na wanakosa maarifa. Ndio maana uanafunzi ni muhimu sana.

> Ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila na ujanja wa wanadamu, katika ujanja tukizifuata njia za udanganyifu. (Waefeso 4:14)

Wakati upepo wa mafundisho au elimu ya mwanadamu unapokuja, tungekuwa bora ikiwa tutajua kile ambacho Biblia inasema. Hatupaswi kuwa watoto tena, bali watu wazima, katika ufahamu wetu wa Neno la Mungu kuhusu ndoa.

## Somo la 2

## Mahitaji ya Wanaume

Mafunzo yetu yanategemea kabisa Maandiko. Katika Waefeso 5: 21-33, tunapata mafundisho ya wazi juu ya mahitaji yetu ya kipekee katika ushirika kama waume na wake. Na tunapoanza mafunzo haya, tukumbuke kwamba mafanikio huja tu kwa njia ya utii, kwa kuitikia sauti ya Roho Mtakatifu, ambaye Yesu alimtuma kukaa ndani yetu, kutufundisha na kutuongoza katika ukweli wote.

> Wala msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe na Roho. (Waefeso 5:18)

Mwandishi mmoja Mkristo anayejulikana aliaandika juu ya Roho Mtakatifu kwa kusema:

> Jazwa na Roho. Kwa hivyo muumini, badala ya kujidhibiti mwenyewe, anadhibitiwa na Roho Mtakatifu. . . na Kristo ndiye dhana ya kujazwa huko (Wakolosai 3:15). Kwa hivyo katika uhusiano huu, muumini anapojitolea kwa Bwana na kudhibitiwa na yeye, anazidi kulidhihirisha tunda la Roho (Wagalatia 5: 22-23). [4]

Hapa tena tunaiona kanuni hiyo, "ikiwa muumini hujitolea kwa Bwana," hiyo huwa kama hali ya kufaulu kwetu. Yeye ni msingi wetu imara na ni kwa nguvu yake ndio tunapata uwezo wa kudhihirisha tunda la Roho na kutimiza mapenzi ya Mungu.

### Kunyenyekeana

Katika Waefeso 5:21, Mungu anasema, "Kunyenyekeana ni kumwogopa Mungu." Kwa nini Mungu anataka tuelewe hili kwanza? Kwa sababu anajua tunapambana dhidi ya ubinafsi, ushindani na shauku ya kutawala kwa kila mmoja. Na hii sio jambo la wanaume tu, la wanawake hufanya hivyo pia. Laana juu ya Hawa, baada ya kula tunda, ilikuwa ni kupambana na shauku ya kunyakua mamlaka ambayo Mungu alimpa mumewe (Mwanzo 3:16).

Baada ya mwanaume na mwanamke kumkaidi Mungu kwa kutumia hiari yao kula kwa Mti wa Ujuzi wa mema na mabaya, wangepata matokeo ya uasi wao. Laana zinazotokana na anguko zimeandikwa katika Mwanzo 3: 16-19.

> Kwa huyo mwanamke alimwambia:
> “Nitaongeza sana huzuni yako na uchungu wako;
> Utazaa watoto wako kwa uchungu;
> Na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye
> atakutawala. ” (Mwanzo 3:16)

Neno *tamaa* katika Mwanzo 3:16, pia katika Mwanzo 4:7, linamaanisha hamu ya kutawala. Mwanaume amepewa mamlaka juu ya mkewe, hivyo baada ya hapo alipaswa kupambania kujinyenyekeza chini ya mamlaka ya mumewe na hata *kutokuwa na haja* ya kutaka kujiinua kwenye uongozi wa mume wake.

**Kila Muumini**

Kwa wanawake ambao wanajitahidi kujionyesha, kwa asili wakitaka kutawala waume zao na kunyakua mamlaka, Mungu anaweza na atawapa neema na nguvu ya kupokea kutokana na mapenzi yake. Waefeso inasema tu, "Kunyenyekeana kwa hofu ya Mungu." Lengo la mstari huo ni "kutangaza bila shaka kwamba kila Mkristo aliyejazwa roho anapaswa kuwa mnyenyekevu na mtiifu. Huu ni msingi wa mahusiano yetu; hakuna mwamini ambaye asili yake ni bora kuliko mwamini mwingine. Katika msimamo wetu mbele za Mungu, sisi ni sawa kwa kila namna (Wagalatia 3:28). " [5] Mstari huu unaweka wazi kuwa Mungu anatuthamini sisi kwa usawa. Kwa mwanamke au mwanaume, hakuna aliye mdogo kuliko mwingine. Hii pia inatupa msingi "katika kumcha Mungu", katika shauku yetu na kujitolea kwa ajili ya wengine na kukidhi mahitaji ya urafiki kwa kila mtu kama vile kwa Bwana.

> Kumcha Bwana ni mwanzo wa hekima,
> Na kumjua Mtakatifu ni ufahamu. (Mithali 9:10)

Lazima tutambue mahitaji ya wenzi wetu ni ya muhimu kwa Mungu kama ya kwetu. Fikiria sauti ya Mungu ikisema, "Kabla sijakuonyesha mahitaji yako ya kipekee ya ushirika, nataka utambue kuwa unawajibika kukidhi mahitaji ya mwenzi wako." Mbele ya Mungu, jukumu letu ni kukidhi mahitaji ya wengine. Huu ni upendo ulio kwa njia ya Mungu.

Waefeso 5:21 inampa kila mmoja wetu changamoto ya kunyenyekea kwa mtu mwingine ili kumtii Mungu. Hii inaonyesha uhiari wa kufanya matendo ambayo Mungu ametuitia kutenda kama mume na mke, kujitolea kwenye mapenzi yake bila kujali jinsi tunavyo *hisi*. Mungu hatumii tu njia ya kuturekebisha na kuwabariki wenzi wetu kiroho, bali pia atatumia utii wetu kutubadilisha kuwa mfano wa Mwanawe, Yesu Kristo, ambayo ni mapenzi yake kwa kila muumini.

Hii ndio tafsiri ya kuwa mwanafunzi: tamaa yetu kubwa ni kumfuata Kristo wakati Mungu anatugeuza kuwa mfano wake. Unaweza kuwa Mkristo, lakini mwanafunzi ameazimiwa kutii kila kitu ambacho Mungu huweka mbele yake.

Watu wengi katika ushauri na saha huwa hawana tamaa ya kutimiza mapenzi ya Mungu. Hawafanyi kazi zao za nyumbani au kufuata mwongozo wa wazi ambao Mungu ameutoa. Ikumbukwe kuwa hakuna uwezo wa maajabu katika hili. Mungu hatafanya kwa muujiza kile ambacho alikuitia wewe kukifanya kwa utii. Mpaka pale utakapojikabidhi kwake na kusema, "Sawa, Mungu nataka kujichunguza mwenyewe, kuona ikiwa ninatimiza mapenzi yako na ninatamani kutii," la sivyo, ndoa yako haitabadilika kamwe.

Ushirikiano wa pamoja ni bora, lakini lazima kila wakati tuelekeze macho yetu kwa Mungu, sio wenzi wetu. Unawajibika kwa utii wako mwenyewe, sio wa mwenzi wako. Haifai kwa mwenzi mmoja tu kujitolea zaidi kubadilika kuliko mwingine. Mara nyingi mwenzi mmoja ndiye huamua kumtii Mungu, jambo ambalo husababisha mwenzake abadilike na kuwa bora pia. Inahitajika mtu kufanya uamuzi huo; lengo la kutimiza majukumu yetu linapaswa kuwa kumpendeza Mungu, sio kupendezana sisi kwa sisi.

**CHIMBA ZAIDI**

Je! Uhusiano kati ya Yesu na Baba uko kama wetu? Je! Yesu alifanya nini kupata uhusiano kama huo na hiyo inawezaje kutumika kwa maisha yako?

> Naye aliyenituma yuko pamoja nami. Baba hakuniacha peke yangu, kwa sababu nafanya siku zote mambo yanayompendeza. (Yohana 8:29)

Je! Ni nini kinachopaswa kuwa msukumo wa utii katika uhusiano wako na Mungu? Unawezaje kuhusisha hii na ndoa yako na mtazamo wako kwa mwenzi wako? Ikiwezekana, chagua eneo maalum la changamoto na uamue jinsi ya kumpendeza Mungu kwa tabia yako.

> Kwa hivyo tena ikiwa tupo hapa au hatuko hapa twajitahidi, kumpendeza yeye. (2 Wakorintho 5: 9)

> Iliyobaki ndugu, tunakusihini na kuwaonya kwamba mwenende katika Bwana Yesu, kama mlivyopokea kutoka kwetu jinsi mnapaswa kuishi na kumpendeza Mungu. (1 Wathesalonike 4: 1)

> Kwa imani Henoko alichukuliwa ili asione mauti, "wala hakuonekana, kwa sababu Mungu alimuhamisha"; kwa maana kabla hajachukuliwa alikuwa na ushuhuda huu, ya kuwa alimpendeza Mungu. (Waebrania 11: 5)

Onyo njiani: Ikiwa utapotoka na kushindwa kurudi kwenye uwezekano wako wa utii na kumtumikia mwenzi wako, basi unakuwa na motisha binafsi na utapata mambo matatu: kukata tamaa, kufadhaika na kudharauliwa. Je! Unatambua hisia yoyote hapa? basi rudi kwenye utii, ukitarajia thawabu yako kutoka kwa Mungu. Mungu si mwongo,atakubariki kama mwanafunzi mtiifu bila kujali tabia ya mumeo au mkeo.

**Kujichunguza 1**

Ikiwa Mungu ametumia habari hii kufunua matarajio yoyote ya ubinafsi au majibu ya dhambi kwa mwenzi wako, ikiri hapo chini na umwombe Mungu akusaidie kuacha.

_______________________________________________________________________
_______________________________________________________________________
_______________________________________________________________________
_______________________________________________________________________
_______________________________________________________________________
_______________________________________________________________________
_______________________________________________________________________
________________________________________________

**Mahitaji ya Ushirika kwa Mwanaume**

Na tuangalie Waefeso 5 ili tujifunze juu ya ushirika wa kipekee ambao Mungu ameweka ndani ya mume. Mungu alibuni ndoa ili kwamba mke ndiye anayemtia moyo mumewe na kumpa msaada ambao ni muhimu katika kukidhi mahitaji ya ushirika wake wa kuzaliwa. Wanaume hawabuni mahitaji haya, yamewekwa ndani yao na Mungu. Hii ndiyo sababu kuna Maandiko yanaonya kuwa tunapokataa kukidhi mahitaji ya mwenzi, tunafungua ndoa zetu kuwa na shida na majaribu.

> Wake, watiini waume zenu, kama kumtii Bwana wetu. Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama vile Kristo pia ni kichwa cha Kanisa; naye ndiye Mwokozi wa mwili. Kwa hiyo, kama vile Kanisa liko limtiivyo Kristo, vivyo hivyo wake na watiini waume zao katika kila jambo. . . . na mke aone kwamba anamheshimu mumewe. (Waefeso 5: 22-24, 33)

**FAILI LENYE UKWELI**

*Tii-Hupotasso* (Kigiriki). Mtazamo wa hiari wa kujitoa, kushirikiana, kuchukua jukumu, na kubeba mzigo.

Kumbuka kwamba kifungu hiki hakisemi tu "watiini," lakini kinaongeza "kama kwa Bwana." Halafu inabainishwa, "kama vile Kanisa linavyomtii Kristo, vivyo hivyo wake na watiini waume zao katika kila kitu." Wanatii kwa waume zao kwa vitu vingapi? Wanawake, katika *kila jambo.* Sio tu vitu kadhaa, lakini kila kitu. Maandiko pia yanaamuru wake kuheshimu waume zao, ambayo leo inamaanisha kumtendea kwa heshima.

Je! Unaona maneno yoyote katika vifungu hivi vya

Maandiko ambavyo huwafanya wanawake wasitii?

**Kujichunguza 2**

Wanawake jichunguzeni muone jinsi mtakavyopokea jambo hili. Je! Unafikiria kuwa mwanaume hastahili, anastahili tu kwa wakati fulani, au kwamba utakuwa wa chini na kwa namna fulani hii haionekani kuwa sawa? ___ Ndio__Hapana

Ikiwa ndio, kiri na muombe Mungu imani ya kumwamini. Tambua wasiwasi wako na uombe moyo mtiifu na hekima maalum ya kuponya kutokuamini kwako.

________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________

Wake, Mungu hakukosea kuweka mahitaji haya kwa mumeo. Inaweza kuwa kuna wakati mwingine Mungu anatutaka tufanye vitu ambavyo vinaonekana kuwa haviwezekani au haviko sawa. Lakini kumbuka, tunaishi katika jamii ambayo inauliza ikiwa maisha ni ya haki na mara nyingi hukataa Neno la Mungu kama jambo lisilo la haki. Tunaweza kuleta mawazo haya katika ndoa zetu, tukiamini hali yetu si haki wakati ni mapenzi ya Mungu. Mabadiliko ambayo yanahitajika kweli ni kujitolea kwetu kumwamini na kumtii. Maisha yataonekana kutokuwa sawa ikiwa tunajizingatia sisi wenyewe na tunaangalia ndani yetu katika kuamua nini tunahitaji kutimiza. Mbali na mtazamo wa Mungu, siku zote tutajisikia kudanganywa kwa sababu mwili hauwezi kuridhika kamwe. Tunaposhika amri zake, tunakaa katika upendo wake na kuwa na furaha.

> Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu, kama vile mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake.
>
> Nimewaambia haya, ili furaha yangu ibaki ndani yenu, na furaha yenu ikamilike. (Yohana 15: 10–11)

Mungu ndiye muumbaji na yeye peke yake ndiye anayeandika mwongozo wa maagizo. Mume wako haelewi ni kwanini ana mahitaji haya maalum na kwanini anahisi kutotimizwa kipindi ambacho mkewe anakuwa hamshughulikii vizuri. Wanaume wengi hawawezi kuelezea mahitaji yao. Baada ya kusoma hii, wataweza kufafanua. Na, wanaume, wakati mnapohisi ubayana, unahitaji kuwa na uwezo wa kumwambia mke wako kwa upendo kile kinachokosekana.

Wanawake, haki na isiyo haki sio kiwango cha utii wetu, lakini tunamtii Mungu kwa moyo wa imani na upendo kwake. Unaweza kuwa na wasiwasi juu ya kujikabidhi kwa mtu huyu maishani mwako, lakini unajitiisha kwa Bwana. Unapofanya hivyo, Mungu ataheshimu utii wako mwaminifu.

Wacha tuweke kando neno la *furaha* kwa sasa. Watakatifu wengi wamemtii Mungu na wamekuwa wasio na furaha sana wakati mwingine. Tunaposoma juu ya maisha ya Yesu, hakika furaha yake ya karibu haikuwa lengo la matendo yake. Na kanuni hiyo hiyo ni

dhahiri katika maisha ya wanafunzi, haswa katika maisha ya mtume Paulo. Bibilia inasema Paulo alipigwa mawe, aliachwa akifikiri amekufa (Matendo 14:19), na akarudi tena kumtumikia Bwana. Katika 2 Wakorintho 11: 23-30, Paulo aliorodhesha mateso na majanga yake bila kulalamika.

Hiyo ni ngumu kuelewa. Utamaduni wetu unaangalia mateso kwa njia mbaya na inayodhalilisha. Lakini haya sio maisha ya muumini kama ilivyoelezewa katika Maandiko. Tunakua bora na wenye nguvu tunapoteseka kwa ajili ya Kristo. Biblia inasema kwamba wakati sisi ni dhaifu, neema yake inatutosha kwa sababu nguvu zake zinatimizwa katika udhaifu wetu (2 Wakorintho 12: 9-10). Kama wanafunzi wa Yesu Kristo, hatupaswi kuruhusu maoni ya ulimwengu na desturi zao ziamuru kile tunachokiamini na kile tunachofanya.

**CHIMBA ZAIDI**

Tambua kile ambacho Maandiko haya yanasema juu ya alama na mateso na matokeo yake katika maisha yetu. Hii ni kanuni ya jumla kwa waume na wake.

> Wala si hayo tu, bali pia tunajisifu katika dhiki, tukijua ya kuwa dhiki huleta saburi; na uvumilivu, tabia; na tabia, tumaini. (Warumi 5: 3-4)

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
__________________________________________________________

> Ndugu zangu, hesabuni kuwa ni furaha tupu mkiangukia katika majaribu mbali mbali, mkifahamu kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. subira iwe na kazi kamilifu, ili mpate kuwa wakamilifu na watimilifu, bila kupungukiwa na neno. (Yakobo 1: 2–4)

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
__________________________________________________________

> Katika hili mnafurahi sana, ingawa sasa kwa kitambo kidogo, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa na majaribu mbali mbali, ili ukweli wa imani yenu, iliyo ya thamani zaidi kuliko dhahabu iharibikayo, ijapokuwa inajaribiwa na moto, inaweza kuwa kupatikana kwa sifa, heshima, na utukufu katika kufunuliwa kwa Yesu Kristo. (1 Petro 1: 6-7)

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
__________________________________________________________

Kabla sijateswa nilipotea, Lakini sasa
nalishika neno lako.
Wewe ni mwema na unatenda mema;
Unifundishe amri zako. (Zaburi 119: 67-68)

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
__________________________________________________________

Ni vema kwangu mimi kuteswa, Ili nipate
kujifunza amri zako.
Sheria ya kinywa chako ni bora kwangu
Kuliko maelfu ya sarafu za dhahabu na fedha. (Zaburi 119: 71-72)

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
__________________________________________________________

Najua, Ee Bwana, kwamba hukumu zako ni
sawa, Na kwamba kwa uaminifu
umenitesa mimi.
Nakuomba, fadhili zako za rehema ziwe faraja yangu,
Kulingana na neno lako kwa mtumishi wako. (Zaburi 119: 75-76)

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
__________________________________________________________

***MPANGO KAZI 1***

Muombe Mungu imani ya kumwamini wakati wa mateso. Mwambie jinsi unavyohisi, mwambie juu ya hofu yako na zungumza naye kwa uaminifu na wazi. Katika Zaburi, Daudi alimwaga moyo wake kwa Mungu, na Mungu alimpenda sana Daudi kwa sababu ya unyenyekevu huu.

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

_______________________________________________

**Vikwazo**

Kuna vikwazo mahsusi vinavyoweza kumfanya mwanamke asitake kunyenyekea kwa mumewe. Wanaume wanaweza kuwa wamefanya uchaguzi wa kibinafsi na kijinga ambao umeumiza hisia za mabinti, wake na wanawake, kama unyanyasaji wa kijinsia, ubakaji, vurugu, kutelekezwa, kutokuheshimu na ukatili. Mwanamke anaweza kuwa amepata moja au zaidi ya haya kutoka kwa baba, kaka, wajomba, majirani, au marafiki wa kiume.

Ikiwa umewahi kupata yoyote ya haya na unajitahidi kuamini jukumu la mumeo katika kukukinga au kuunga mkono uongozi wake kama baba, suala hili linaweza kukusababishia wasiwasi au hofu. Labda huwezi hata kufikiria kuweza au kutaka kuwa mke ambaye Mungu anakuita uwe. Labda baba yako alimwakilisha vibaya Mungu na kukuumiza wewe, mama yako, kaka zako, au dada zako na hiyo imeathiri sana moyo wako kuhusiana na wanaume. Labda unahisi kama umeolewa na mtu ambaye hajui anachofanya. Moyo wako unaweza kuwa unaumia na unafikiria, *nitakua nimelaaniwa ikiwa nitamtii mjinga huyu*. Unaweza umejaa machungu ya zamani, ukipambana na uhasama na kujilinda badala ya kumwamini Mungu, kuonyesha uhitaji na kudhibitisha uongozi wa mumeo.

Je! Unajikuta unashambulia kwa hasira au matusi wakati mumeo anajaribu kuongoza? Unaweza kudhani anajaribu kukudhibiti. Hii ni hisia ya kawaida ikiwa haujawahi kushughulikia machungu yako ya zamani. Chukua muda wa kuomba, "Mungu, je! Ninahitaji kutafuta uponyaji kupitia msamaha kwa sababu ninajitahidi kukuamini na kujitoa kwa uongozi wa mume wangu? Bwana, sina hakika hata ninaweza kukuamini katika hii. " Hili sio suala la kutotii kila wakati, lakini mara nyingi ni kwa sababu ya maisha ya nyuma ambayo hayajashughulikiwa kibiblia.

Ikiwa hii imekugusa kwa sasa, lazima urudi nyuma juu ya maisha yako ya nyuma. Chunguza ni wapi unahitaji kutafuta uponyaji na ni nani unahitaji kumsamehe. Njia mbadala ni kuishi katika hali ya dhambi ya uchungu na kutokuwa na uwezo wa kuamini, ambayo itaambukiza kila mtu karibu nawe.

> Tafuta kwa bidii kuwa na amani na watu wote, na utakatifu ambao hakuna mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao: mkiangalia sana mtu akapungukiwa na neema ya Mungu; shina la uchungu lisije likachipuka likawasumbua na watu wengine wakatia unajisi kwa hilo. (Waebrania 12: 14-15)

Maumivu ambayo wengine wametusababishia yanaweza kuwa ngome na minyororo ambavyo huweza kuzuia maendeleo yetu ya Kikristo; tutapona tu pale tutakapowasamehe. Lazima utumie dawa ya msamaha kwa maisha yako ya zamani. Nenda kwenye *Kiambatisho P: Uaminifu na Msamaha* na ufuate kanuni zilizowekwa kwako.

Mpango wa Mungu kwa mke ni kwamba kwanza mke aweke imani yake kwa Mungu. Hii inamaanisha kujitoa kwa ajili ya mpango wake wa kutimiza mahitaji ya ushirika wa mumewe na sio mahitaji ya mila zetu, tamaduni, kabila, machungu ya zamani, au hata njia ambayo wazazi wetu waliishi na kutupasa kuongozwa nao. Mwongozo lazima uwe Neno la Mungu.

***MPANGO KAZI 2***

Andika ahadi ya kuomba kusoma kiambatisho cha msamaha na upatanisho, ikiwa inahitajika. Fuata kila hoja kwa hatua inahitajika. Mwanamke mkorofi huweza kutavunja nyumba yake mwenyewe hata pasipo kukusudia.

Tafadhali kumbuka: Ikiwa kwa sasa unapambana katika uhusiano wenye unyanyasaji, lazima utafute msaada. Ni muhimu kujua kwamba Mungu wala sisi hatukubali unyanyasaji kwa njia yoyote. Ikiwa unyanyasaji wa mwili au matusi upo, tafuta msaada unaofaa. Inapendekezwa mtu mwingine kuingilia kati kwa ajili ya ushauri.

## Somo la 3

## Jihadharini na Ushawishi wa Kidunia

Je! Umekuwa ukiacha mawazo na tabia yako vididimizwe na ushawishi wa falsafa za ulimwengu? Ikiwa ndivyo, hiyo inaweza kuwa imeambukiza ndoa yako pia. Watu wengi katika ushauri na saha wanasema, "Kweli, katika tamaduni yangu (kumaanisha asili ya kabila), hii ndio njia tunayofanya." Au "Kama __________ (jaza yako asili ya kikabila), mwanamke hana neno nyumbani, au mwanamke hufanya mafunzo yote ya watoto. " Lakini kama Wakristo, lazima tuweke imani zetu za kitamaduni kando, kwa sababu zinapingana moja kwa moja na Neno la Mungu. Mara nyingi, imani za kitamaduni ni mapendeleo tu bila kuhusisha maadili, na ni sawa kabisa kuzifuata; lakini, wakati imani ya kitamaduni inapopingana na Biblia, huleta mgongano wa maadili, ambayo ni dhambi. Lazima *kila wakati* tuangalie imani zetu juu ya ndoa na familia kwa kuvihusisha na Neno la Mungu.

### Ushawishi wa Kitamaduni

Utamaduni wetu, au falsafa na kanuni za ulimwengu huu vinatuzunguka; hekima ya ulimwengu huja kupitia media (vitabu, Runinga, sinema, majarida na mtandao, kwa kutaja machache tu) au mara nyingi kupitia elimu na shinikizo la rika. Yoyote ya haya yanaweza kutushawishi kutazama ndoa na familia kupitia mwangaza wa ulimwengu. Imani na falsafa zinaweza kuzama sana kiasi kwamba tunaamini kuwa ni kweli hii ndiyo njia ya kuendesha ndoa, hadi tutakapoilinganishe na Neno la Mungu.

### Mila za Kidini

Mafundisho mengi ya dini kuhusu ndoa na malezi vimekuwa kama mila. Badala yake, tuwe kama Wakristo wa Berea, ambao baada ya kusikia mafundisho ya Paulo, "walichunguza Maandiko kila siku ili kujua kama mambo haya ni kweli" (Matendo 17:11). Usichukue neno la mtu mwingine kwa upofu juu ya ukweli, hata kutoka kwa kitabu hiki cha kujifunzia, badala yake fungua Neno na uhakikishe kuwa ni kweli. Yesu alilazimika kushughulika na viongozi wa dini ambao walipendelea kuishi maisha yao kulingana na mila ambayo ilitawala utamaduni wa kidini ambao walilelewa nao. Kwa kukataa kwa ukaidi kuacha mawazo hayo waliyofundishwa na wanadamu, mwishowe walimkataa Mwokozi ambaye alikuja kuwaokoa.

### Mila ya Wanaume

Mila ni imani na tabia ambazo hupitishwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine, kizazi kimoja hadi kingine. Wazazi huwapa watoto ushauri mbaya wa ndoa wakitumia maisha yao kama kipimo. Lakini Wakristo lazima wafanye maamuzi magumu linapokuja suala la kumfuata Kristo. Wakati Neno la Mungu linapokuwa ni kipimo chetu, lazima kila mara tumweshimu Mungu na Neno lake juu ya wengine wote, pamoja na wazazi wetu. Tuna falsafa za zamani, wanasaikolojia wa sasa, na waandishi wengi waliochapishwa juu ya mada ya ndoa. Wengine wamekuwa kama mkondo mkuu wa mawazo juu ya ndoa na malezi. Wanaume kama Sigmund Freud bado wanazingatiwa kama chanzo kinachofaa cha habari. Wengi wa watu hawa hawakufanikiwa hata wao binafsi, hawajaweza kuyatimiza hayo. Kamwe usifuate ushauri ambao haujathibitishwa na Neno la Mungu. Yesu alitoa onyo nzuri juu ya mada hii.

> Akawambia, vema mwaikataa amri ya Mungu, mpate kuyashika mapokeo yenu . . . mkilitangaza Neno la Mungu kuwa mapokeo yenu mliyopokeana. Tena mwafanya mambo mengi yaliyo sawasawa na hayo. (Marko 7: 9, 13)

Mungu alikuwa amewapa Wayahudi maagizo ya kuishi, lakini viongozi wao wa kidini walikuwa wamebadilika, wakageuka na kuongeza katika Maneno yake mpaka walipowatia watu chini ya sheria au kanuni zilizotengenezwa na wanadamu , ambazo sio ukweli. Kwa kufanya hivyo, walilifanya Neno la Mungu kutokuwa na matokeo. Katika muktadha huu, Mafarisayo walikuwa wakisema kwamba hawawezi kuwatunza wazazi wao kifedha kwa sababu pesa hiyo ilikuwa "korban," zawadi ya dhabihu kwa Mungu. Kwa kweli, walikuwa wakidumisha uchoyo, wakiokoa pesa hizo kwa malengo yao wenyewe.

Hii inaonyesha jinsi mioyo yetu inavyoweza kuwa ya udanganyifu, ili tupate kupenyeza mawazo yetu wenyewe kwenye Maandiko katika kutoshea malengo yetu wenyewe. Yesu alisema, "Wananiabudu bure, wakifundisha mafundisho ya amri za wanadamu" (Marko 7: 7). Hakuna neno au tendo ambalo linaonekana na Bwana.

**Mila ya Kibiblia**

Kuna mila ambayo tunapaswa kushikilia sana. Paulo aliliambia Kanisa la Thesalonike, "Kwa hiyo, ndugu zangu, simameni imara na mkashike mapokeo mliyofundishwa, iwe kwa neno au barua yetu" (2 Wathesalonike 2:15). Paulo alikuwa anasema simama imara na ushikilie kweli za kibiblia ambazo walikuwa wamepewa na mitume kupitia mahubiri na barua zao. Lazima sote tuushike kwa bidii ukweli.

Hatuwezi kuruhusu uhusiano mwingine wowote utusababishe tupoteze ukweli katika Kristo, bila kujali jinsi inavyoweza kuonekana kwa wengine. Na kama Wakristo, wakati mwingine tutachukuliwa kuwa wa ajabu wakati tunapofuata kanuni za kibiblia ambazo ni kinyume na maoni ya ulimwengu.

> Mambo ambayo wao huona ni ya ajabu ninyi kutokwenda mbio pamoja nao katika ufisadi ule ule usio na kiasi, wakiwatukana. (1 Petro 4: 4)

Tunapaswa kuonekana wa ajabu, kwa sababu sisi ni wageni, wageni kwenye mambo ya ulimwengu, kwa kuwa Neno la Mungu sasa linaamuru na kutawala kila kitu tunachokifanya.

> Kwamba zamani zile mlikuwa hamna Kristo, mmefarakana na jamii ya Israeli, wageni wa maagano ya ahadi ile. (Waefeso 2:12)

**Kujichunguza 1**

Je! Kwa njia yoyote unafuata utamaduni au mila ya kidini ambayo haikubaliani na Neno la Mungu? Inaathiri ndoa yako? Jadili hili kama mume na mke. Andika kile ulichojifunza kutoka kwa kila sehemu hapo juu.

______________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________________

______________________________________________________________

**Mtazamo wa Yesu juu ya Familia**

Yesu alionya juu ya kuweka maoni au ushawishi wa mtu yeyote mbele ya Mungu aliposema, "Mtu yeyote akija Kwangu na asichukie baba yake na mama yake, mke na watoto, kaka na dada, naam, na maisha yake mwenyewe pia, hawezi kuwa Mwanafunzi wangu ”(Luka 14:26).

Yesu hasemi kwamba kumpenda lazima uchukie mwenzi wako, watoto, na watu wengine wa familia. Badala yake, ikiwa inakuja uchaguzi wa kufanya kitu kwa njia ya Mungu au njia ya wazazi wetu, au ya ulimwengu au njia yetu wenyewe, lazima tuchague njia ya Mungu. Neno lililotafsiriwa katika mstari huu kama *chuki kwa* kweli linamaanisha "penda kidogo." Upendo wetu kwa Mungu, Neno Lake, na kile Anachotaka ni kuwa kubwa kuliko kujitolea kwengine kokote. Kumtii Kristo kwa gharama yoyote ile ni tabia ya mwanafunzi wa kweli. Katika siku za Kristo, Wayahudi ambao walichagua kumfuata Kristo, kujitambulisha hadharani kama wanafunzi Wake, walizuiliwa na kuadhibiwa. Hii bado inatokea ulimwenguni kote kwa wale wanaomchagua Kristo.

Ikiwa hatutii Mungu na kuchagua kumpenda kidogo, kuna matokeo. Kwanza, amani hupotea, kisha furaha, kisha kuridhika, na mwishowe matunda ya kiroho. Tunda la Roho, ambalo ni upendo, halitakuwa likitiririka kutoka kwako, bali matunda ya mwili wako. Matunda *hayo* ni mazuri kiasi gani? Ni nyama iliyooza. Biblia inasema kwamba haki zetu zote za kujifanya ni kama matambara machafu kwa Mungu.

> Lakini sisi sote tumekuwa kama kitu kilicho najisi,
> Na haki zetu zote ni kama matambara machafu;
> Sisi sote tunakauka kama
> jani, Na maovu yetu, kama
> upepo;Wametuchukua.
> (Isaya 64: 6)

Hakuna kitu kizuri kinachotoka kwetu-hata kitu kimoja kizuri. Na tunapojikuta katika hali hii, wakati sisi ni duni na wenye huzuni na tuna taka hii yote ikitutoka, je! Sisi kawaida hufanya nini kama wanadamu? Tunalaumu wengine kwa mitazamo yetu mibaya na tabia mbaya, kana kwamba majibu yetu ni ya kawaida na yana haki chini ya shinikizo la kutisha kama hilo.

Waume na wake hufanya hivyo. Angalia Adamu na Hawa. Mungu aliingia ndani ya bustani baada ya kula tunda lililokatazwa na kuuliza, "Adam, ni nini kilitokea?" Maneno gani ya kwanza kutoka kinywani mwa Adamu? "Ni yule mwanamke uliyenipa." Alijaribu kulaumu Mungu-na mkewe. Ni asili yetu ya dhambi.

Waume na wake kawaida humlaumu mtu mwingine kwa shida zao. Watu walio katika dhambi, wakifanya kwa njia yao wenyewe kulingana na uelewa wao wenyewe na hawajui au kufuata maagizo ya Mungu, ni wanyonge.

Ukiruhusu macho yako yajazwe na kutofaulu kwa mwenzi wako, hautaona wazi kabisa. Lazima uone dhambi yako mwenyewe, utubu, na umfuate Mungu kwa utii.

Mungu anatuambia tena na tena, "Amini njia yangu, usitegemee ufahamu wako mwenyewe. Amani na furaha hutoka Kwangu. " Sio mume wako, sio mke wako, na sio kutoka kwako. Uko katika dhambi wakati unafanya kwa njia yako mwenyewe, na utakuwa mnyonge kwa sababu Yeye anakupenda sana kukuruhusu ufurahi.
Mungu anasema anamwadhibu kila mmoja wa watoto wake kwa sababu ya upendo wake mkamilifu kwetu (Waebrania 12: 5-6).

Ishara ya kwanza ya nidhamu ni kupoteza amani, furaha, na kuridhika. Majonzi hufuata. Na kisha matunda ya mwili wetu huanza kuchanua. Badala ya kuendelea kulaumu, suluhisho pekee ni kumtafuta Mungu na kuwa tayari kujichunguza. Lazima tuache kuchunguza matunda ya mwenzi wetu na tuangalie yetu wenyewe.

**Kujichunguza 2**

Ikiwa umezingatia kwenye au kumlaumu mwenzi wako kwa kutokuwa na furaha kwako, andika ukiri wa maombi kwa Mungu, ukimuomba afunue dhambi yako na akubadilishe.

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
__________________________________________________________

Pamoja na kuweka kando falsafa zingine na kuondoa tabia za lawama, tuwe tayari kukitafuta kile ambacho Mungu anakisema. Mahitaji ya ushirika ya mume yamelala kimantiki chini ya maagizo ya Mungu kwa mke. Mungu anawaambia wake wote: Tiini kama kwa Bwana, kwa maana kwamba mume wako ni kichwa. Kuwa chini ya mume wako kwa kila kitu; muheshimu na kumthamini mumeo. Je! Hiyo yote inamaanisha nini katika maisha ya kila siku?

**Kazi ya kunyenyekea: Kuthibitisha mamlaka ya Mumeo**

Je! Unahisi kuwa mume wako hajui kuongoza na yaliyopita yamejaa makosa yake? Inaeleweka, kwa mtazamo wa kibinadamu, kwamba ungekuwa na mashaka juu ya kunyenyekea kwa mtu huyu, ukimwamini Mungu kweli kujiweka chini ya mamlaka yake. Biblia inaelezea jinsi hii inavyoonekana, asili ya mwanamke mtiifu.

> Kadhalika ninyi wake, watiini waume zenu wenyewe, kusudi ikiwa wako wasioliamini Neno, wavutiwe kwa mwenendo wa wake zao, wakiutazama mwenendo wenu safi na hofu. Kujipamba kwenu kusiwe kujipamba kwa nje, yaani kusuka nywele, kujitia dhahabu, au kuvaa mavazi mazuri; bali uwe ni utu wa rohoni usioonekana katika mapambo yasiyo; yaani roho ya upole na utulivu, iliyo thamani kuu mbele ya Mungu. Maana hivyo ndivyo walivyojipamba wanawake watakatifu wa zamani, waliomtumaini Mungu na kuwa kitii waume zao. Kama vile Sara alivyomtii Ibrahimu, akimwita bwana, nanyi ni binti zake, mkifanya mema wala hamkutishwa kwa hofu yoyote (1 Petro 3: 1-6)

Kumbuka mistari hii imeelekezwa kwa wanawake walio na waume ambao hawatii Neno. Hakuna asiyehusika juu ya kutii, kwa kuwa mafundisho kwa mke ni maalum kabisa na endelea kuwa mtiifu. Mstari huu inashughulikia uwezekano wa mke kushawishi mume asiyeamini kuelekea ushirika na Bwana ("anaweza kushinda"). Nguvu ya mke iko katika

mwenendo na mtazamo wake, sio maneno ("bila neno"). Weka tumaini lako kwa Mungu, jikabidhi kwenye mapenzi yake kama mke, naye atafanya kazi hiyo.

Wanandoa wengi wana mwenzi mmoja asiyeamini au yule ambaye hutii Neno, jambo ambalo sio rahisi kwao. Mungu anaahidi baraka, lakini si kwa njia rahisi. Wakati mwingine tunakosa mistari inayozungumzia kujikana mwenyewe, msalaba na kukana maisha yako ili kumfuata Yesu (Mathayo 16: 24-25).

Wakati mumeo anapofanya uamuzi wa kijinga au uamuzi mbaya, ambao huukubali, amini kwamba Mungu haukubali pia ("hata kama wengine hawalitii neno" kutoka 1 Petro 3: 1). Tabia ya asili, tangia tulipopata laana kwa uovu, ni kujadili na kubishana mpaka umshinde kwa mtazamo wako. Biblia inasema kumshinda mume "bila Neno" (mstari wa 1). Ni jambo ambalo mmoja husema, "Mpendwa, katika hii kuna njia nyingine ya kuiangalia, lakini nitafuata uongozi wako na uamuzi wako kama mume." Ingawa pia haifai kabisa kujadili au kuendesha jambo kwa hasira kali, vitisho vya kujihami na tabia isiyo ya uthibitisho kama kejeli, ukosoaji, uchungu na kukataliwa. Mke Mkristo anapaswa kuwa anamuombea mumewe ili aweze kuwa kiongozi wa kimungu au kuokolewa, akiamini kwamba Mungu anamtazama kama binti yake na anamjali.

Wake, lengo la Mungu ni kwamba mume wako "ashawishike kwa matendo." Katika muktadha wa 1 Petro 3: 1-6, yeye anafunua muundo wake ili mume "apate" kushawishika na kuvutika kwa matendo ya mkewe. Kumbuka hii sio ahadi, lakini ni njia ambayo Mungu anaweza kufanya kazi kupitia wewe kumleta mume wako kwake. Pia kumbuka kuwa hakuna kikomo cha wakati juu ya kufuata mpango wake. Ndoa nyingi zilizokuwa zinakaribia talaka; kwa karatasi kuwekwa tayari, hugeuzwa kabisa wakati mume na mke wanapofuata mpango wa Mungu. Waume wameokolewa, waamini wamepewa msukumo wa kujifunza na kukua kiroho na marejesho kwa familia nzima yametokea. Mungu ni mwema sana!

Wake, watiwe moyo. Mpango wa Mungu ni kwamba waume "washawishike kwa mienendo ya wake zao, watakapoona mwenendo wako safi" (1 Petro 3: 1-2). *Kuchunguza* namna "kutazama, kuona na kutafakari." [6] Kupitia upya mambo ambayo tumejifunza, Mungu aliumba mwanamke kuwa msaidizi, na mume atajifunza (kwa kutazama, kutafakari, na kuangalia juu ya mwenendo wa mke wake) kwa kuwa yeye anamsaidia. Mwenendo safi unamaanisha kujiepusha na tabia zote kwa mumeo ambazo ni kinyume na mapenzi ya Mungu. Mwandishi mmoja anasema kwamba mke anaweza kuwa na "mambo katika mwenendo wake na hasira yake ambayo yanaweza kuharibu uzuri wa uchaji wake na kuzuia ushawishi wowote mzuri kwenye akili ya mumewe." [7] Mke ana ushawishi mkubwa juu ya mume wake, kumuongoza kwa Mungu, au kumuondoa.

Je! Mke hutimizaje utii huu? Huanzia moyoni. Petro wa Kwanza 3: 3 inazungumza juu ya wasiwasi wa asili wa mwanamke kuhusu nywele zake, vito vya mapambo, na mavazi (leo tunaweza kuongeza mapambo), ambayo ni sawa kwa mtazamo unaofaa. Marehemu J. Vernon McGee, mchungaji aliyejulikana, alisema, "Ikiwa zizi linahitaji uchoraji, lipake rangi." Lakini Mungu, katika mstari wa 4, anafafanua uzuri halisi na tabia ya kike kama, "badala yake iwe utu wa rohoni uliofichika, na uzuri usioweza kuharibika wa roho ya upole na utulivu, ambayo ni ya thamani sana machoni pa Mungu." Mungu anataka tufanye upya akili zetu (Waefeso 4:23) na tuimarishe utu wa ndani (Waefeso 3:16), kwa kuwa mioyoni mwetu hutoka masuala ya maisha (Mithali 4:23) na matendo yetu (Mathayo 15: 18–18) 19).

Wake, elezeni kile "cha thamani sana machoni pa Mungu"  maana ya hii ipo katika 1 Petro 3: 4.

______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
_________________________________________________________________

Tambua kuwa Mungu anaangalia. Mke anapokuwa na tabia nzuri, "ni ya thamani sana" machoni pa Mungu (1 Petro 3: 4). Mungu anataka mwanamke ajue kwamba ikiwa moyo wake ni mnyenyekevu (mtiifu, mpole, na mvumilivu), ikiwa ana roho tulivu (tulivu, isiyosumbuliwa) na ikiwa yuko tayari kuwasilisha, hali hiyo ni ya thamani kubwa kwake. Mungu aliumba mwanamke kwa uhusiano maalum na mwanaume na wakati alipopanga jukumu la mke / msaidizi, alijua yuko tayari kujitiisha kwenye mpango wake mkamilifu, Mungu amebarikiwa na moyo wake na shauku yake ya kumtukuza.

Tunapozungumza juu ya kumtukuza Mungu, hii haimaanishi kuwa ni shauku ya kujisifu au ya kujigamba kwa mamlaka yakiungu. Ni kumfunua Mungu ambaye ni upendo, kuonyesha kwamba ana mema yetu tu katika mawazo yake wakati wote na anasubiri kubariki viumbe vyake kwa kuwajua kwa karibu zaidi kadiri muda unavyokwenda.

## Somo la 4

## Mke anayethibitisha Mamlaka

Wanawake, lazima mlinde mioyo yenu. Mnashambuliwa na magazeti, vitabu vinavyoitwa vya Kikristo, vipindi vya Runinga, vituo vya redio, washauri na makanisa potofu, ambayo yote yanapendekeza usimfanye mume wako kipaumbele. Sinema nyingi huonyesha wanaume kama wababaishaji, wenye ubinafsi na wajinga; lakini picha hii ni sumu kutoka shimo la kuzimu ambalo linaathiri utamaduni wetu. Ingawa tunaiita burudani, vipindi vyetu vingi kwenye Runinga ni kanisa la Shetani. Ikiwa unatazama sinema hizi, acha na usirudi tena.

> Ambao wakijua sana hukumu ya haki ya Mungu, ya kwamba wayatendayo hayo wanastahili mauti, wanatenda hayo wala si hivyo tu bali wanakubaliana nao wayatendao. (Warumi 1:32)

Mungu anataka utumie ushawishi wenye nguvu ambao amekupa kama mke kumsaidia mumeo kuamini kwamba Mungu amemtia mafuta kama kiongozi. Amini kwamba Mungu atampa kila kitu anachohitaji kukua na kujifunza jinsi ya kuifanya kazi hiyo vizuri. Unapaswa kutafuta njia za kumthibitisha kama mumeo. Usimpe mumeo umuhimu mdogo kuliko watoto, nyumba, wanyama, kazi yako, au masilahi yoyote maishani mwako. Wanaume wengi huhisi kama namba sita au saba kwenye orodha ya vipaumbele vya wake zao, lakini kumtunza mumeo ni lazima iwe kipaumbele chako cha *pili* (Waefeso 6:22). Huwezi kubadilisha mpango mkamilifu wa Mungu na *kuto* kumtarajia kupata adhabu; wala hatuwezi kutarajia baraka kwa kutotii.

Ikiwa mume wako anahisi kutothaminiwa, anaweza kuwa na mwitiko mbaya. Na ikiwa unamtendea vibaya, iko wapi baraka na raha ya kuwa na rafiki anayempenda?

Kihistoria, kumekuwa na mkanganyiko mwingi juu ya kile ambacho Mungu anamaanisha kweli kwa mwanaume kua kichwa, au uongozi. Kila tamaduni inakabiliwa na changamoto ya kuelewa na kufuata nia ya kweli ya Mungu katika Maandiko. Kumbuka kwamba ni ule wakati tu tunapogeuza na kuifanya kweli yake ifuate tamaa zetu wenyewe ndipo tunapopotoka. Mchungaji Skip Heitzig, katika ujumbe uliopewa jina la "Mtengenezaji Nyumba au Mvunjaji wa Nyumba," alitoa historia ya zamani juu ya familia wakati wa Kanisa la karne ya kwanza, akionyesha jinsi ushawishi wa kitamaduni unavyoweza kuingia katika maisha yetu.

> Katika ulimwengu wa zamani, miaka elfu mbili iliyopita katika Rumi na Uigiriki, au "Tamaduni ya Wagiriki," kulikuwa na msimamo mkali katika familia. Kwa upande mmoja, ulikuwa na mfumo dume na upande mwingine, ulikuwa na nadharia ya utetezi wa haki za wanawake ya wapagani. Zote mbili zilikuwa nguvu kali. Kweli kwa wingi na uwezo, kwa miaka elfu mbili iliyopita wanauma walikua ndo viongozi pekee. Kwa mantiki hii wanaume wa Kirumi wangaweza kuwa madhalimu kwa sababu kweli kulikuwa na sheria ambayo iliandikwa na Mrumi aliyeitwa "Patria Potestas," au sheria kamili ya mume / baba, ikifafanua kuwa mume ndiye alikuwa anasimamia kabisa maisha na masuala ya familia yake .

Hii inaonekana haiwezekani kutokea kwetu, kwamba watu wanaweza kuhalalisha tuweze kuishi kama hivi. Lakini tunahitaji kutambua kwamba chochote kinaweza kutokea wakati

tunapompuuzia Mungu na Neno lake. Mchungaji DL Moody, mhubiri mashuhuri wa Bwana, alishirikisha uzoefu wake kwa kuonyesha nini kinaweza kutokea pindi tunayapofuata kweli maagizo ya Mungu.

Baada ya ibada Moody alifuatwa na mwanamke na kumwambia, "Unajua, mchungaji, mume wangu sio muumini. Anakunywa pombe, anatukana na nimefanya kila kitu unachoweza kufikiria kumfikisha kanisani na wala hajaja. Nimefanya kila kitu. ” Aliendelea na kuendelea, mambo yote ambayo alijaribu kufanya, asilimia 99 yalikuwa si ya ki Mungu.

Kwa hivyo Moody alimwongoza kwenye 1 Peter na akasema, "Nataka uende nyumbani ufanye hivi."

Asubuhi iliyofuata, aliamka mapema badala ya kukaa kitandani, akampikia kifungua kinywa na akamtengenezea chakula cha mchana; hii iliendelea kwa wiki kadhaa. Kisha akaanza kuandaa samaki kwa chakula cha jioni, samaki amabye yeye mke alimchukia, lakini mme wake alimpenda. Hii iliendelea na siku moja akamwambia mumewe, “Mpendwa, Kanisa linafanya mikutano maalum Jumatano usiku kwa wiki kadhaa zijazo. Naweza kwenda? ”

Mumewe alimwangalia na kusema, “Unaniuliza? Ni lini umewahi kuomba ruhusa ya kwenda kanisani? ”

"Kweli, ni katikati ya wiki na nilitaka kukuuliza," mke alijibu.

Wiki moja ilipita, na mumewe alikuja nyumbani kutoka kazini, akaoga, na akavaa nguo zake nzuri.

"Unafanya nini?" mke alisema.

"Ninatoka,"mume alisema.

"Unamaanisha nini kwenda wapi?" mke alihoji kwa mashaka.

"Mwanaume yeyote aliyeweza kumfanya mke wangu abadilike kiasi hiki anafaa kusikilizwa!" mume alijibu.

Alikuwa amejaribu kila kitu kwa njia yake mwenyewe, lakini alipofuata Neno la Mungu, mumewe alibadilika. Tunahitaji wake zetu kututhibitisha, *sio* kutukumbusha juu ya kufeli kwetu. Tunahitaji kujua wanaamini, sio tu ndani yetu, lakini katika nguvu ya Mungu kutubadilisha tuwe waume ambao Mungu anataka tuwe.

Wake, ikiwa mienendo yenu na mitazamo yenu haionyeshi hili, basi sio tu kwamba haujatimiza hitaji la ushirika la mume wako kama mwanaume, pia unamuasi Mungu. Je! Unatumia ulimi wako na matendo yako kumhukumu mumeo au kumbariki na kumdhibitisha? Biblia inasema wema wa Mungu ndio unatupeleka kwenye toba.

Ni muhimu kutaja hapa kwamba Mungu wala sisi hatukubali unyanyasaji kwa njia yoyote. Ikiwa unyanyasaji wa mwili au matusi upo, tafuta msaada unaofaa. Inapendekezwa apatikane mtu wa kuingia kati kwa ushauri.

Ingawaje wanawake wengi wanasema, "Siwezi tu kuvumilia unyanyasaji; haijalishi hata nimwambie afanye nini, hatanisikiliza. Hatafanya hivyo. ” Tafadhali kumbuka kuwa sio

unyanyasaji wakati hatafanya kile unachotaka afanye. Majaribio kama haya sio unyanyasaji.

Mungu hutumia watu wengine, haswa mwenzi wako, kukupa changamoto na kukukamilisha, kufunua dhambi yako mwenyewe. Mungu hutumia hali ngumu kwenye ndoa yako kukubadilisha na kukupa nafasi ya kujiangalia, usimlaumu mwenzi wako kwa tabia mbaya bila kuvaa kiatu chake. Bila kumwomba Mungu akusamehe na kuomba msamaha kwa mwenzi wako, basi hautabadilika.

**Je! Habari Hii imepitwa na Wakati?**

Wengine wanasema tuko katika karne ya ishirini na moja na mambo yamebadilika, kwa hivyo tunahitaji kuiboresha Biblia ili iende sambamba na nyakati zetu. Biblia imejidhihirisha kuwa chanzo cha ukweli katika kila karne na tamaduni, pamoja na tamaduni zetu pia; k*amwe* haitakuwa imepitwa na wakati.

Ili kuonyesha kwamba dhana ya kwamba uongozi wa mume na utii wa mke haubadiliki kulingana na muda, na tuangalie 1 Petro 3: 1-7. Wakati Petro alipoandika barua hii, ilikuwa karibu mwaka wa 64 BK, zaidi ya miaka elfu mbili iliyopita. Aliwahimiza wake kuwa watiifu kwa waume zao (mstari wa 1 - 4), na kisha akatumia hadithi ya Ibrahimu na Sara kuelezea hoja yake: “Kwa maana kwa njia hii, katika nyakati za zamani, wanawake watakatifu waliomtumaini Mungu pia walijipamba wao wenyewe, wakitii waume zao, kama vile Sara alivyomtii Ibrahimu, akimwita bwana, ambaye ninyi ni binti zake mkifanya mema na msiogope kwa hofu yoyote ”(1 Petro 3: 5-6).

Ibrahimu na Sara waliishi karibu miaka elfu mbili kabla ya barua hii kuandikwa, na Adamu na Hawa waliishi miaka elfu mbili kabla ya hapo. Tukifuata ratiba kutoka kwenye uumbaji: Mungu alimtengenezea Adamu aongoze na Hawa amsaidie. Miaka elfu mbili baada ya hapo, Ibrahimu na Sara walifuata mtindo huo huo. Miaka elfu mbili baadaye, Petro aliwaelekeza waamini wa Agano Jipya kufuata mtindo huo huo. Miaka hiyo elfu nne haikubadilisha jinsi Mungu alivyobuni ndoa ifanye kazi. Ikiwa Mungu angebadilisha mtindo wa usimamizi, angefanya katika Agano Jipya. Na kwa kuwa Neno la Mungu limekamilika na hatupaswi kuongezea au kupunguza kutoka kwake (Kumbukumbu la Torati 4: 2; 12:32; Mithali 30: 6; Ufunuo 22:18), basi tunahitaji kulikumbatia tu.

> Hamtaongeza kwa neno ninalowaamuru, wala msichukue kutoka kwao, mpate kuzishika amri za Bwana, Mungu wenu, ninayowaamuru. (Kumbukumbu la Torati 4: 2)
>
> Usiongeze kwa maneno yake,
> Asije akakukemea ukaonekana mwongo. (Mithali 30: 6)

Hatupaswi kusahau kwamba sisi sote huzaliwa na asili ya dhambi ambayo inataka tumfuate Shetani, ulimwengu, au mwili. Ikiwa hatuko macho, tunaweza kuchafua mtindo wa usimamizi wa Mungu na falsafa ambazo ni kinyume na Maandiko. Lazima tupime kila wazo na hatua dhidi ya Neno lake la thamani. Maombi ya kijinga hayatazuia matokeo mabaya kutokea.

**Maoni ya Mwanamke aliyefanikiwa**

Ikiwa unakumbuka sinema ya TV iitwayo *Full house* , DJ wake akiwa Candace Cameron (kwa sasa, Bure) ambaye kaka yake, Kirk Cameron, aliigiza akiwa katika *Maumivu ya makuzi.* Bado anaigiza na amefanikiwa pia kama mke na mama. Candace alikutana na

mumewe, Val Bure (mchezaji wa Hockey wa Urusi), kwenye mchezo wa Hockey wa hisani na hakuchukua muda baada ya kuolewa akapata watoto. Baada ya kuolewa miaka kumi, hiki ndicho alichosema juu ya ndoa na mtindo wa usimamizi wa Mungu.

Kama ilivyo ndoa yoyote, tumekuwa na siku zetu za furaha na maumivu yetu endelevu(hayakusudiwi), lakini haikuwa rasihi, mpaka ilipofikia karibu miaka kumi katika ndoa yetu ndipo nilianza kuelewa athari ambayo ipo katika jukumu langu kama mke katika umoja huu. Pamoja na mabadiliko yangu mwenyewe, nilifurahi kutambua kuwa uhusiano mzuri uliopo unaweza kubadilishwa kuwa mzuri zaidi

Hatua ya kwanza niliyochukua ni kuelewa kuwa ingawa ndoa ni uhusiano sawa ambapo mume na mke wana umuhimu sawa, hatujaumbwa kushiriki majukumu sawa.

Nikiwa nimeshikilia Biblia, nilisoma, "Maana mwanamume hatoki katika mwanamke; bali mwanamke kwa mwanamume. Wala mwanamume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke; lakini mwanamke kwa ajili ya mwanamume "(1 Wakorintho 11: 8-9).

Jamii ya leo ilinifanya niamini kwamba hakupaswi kuwa na tofauti kati ya mwanaume na mwanamke, katika hili jamii ilikuwa na makosa. Val na mimi tuliumbwa sawa lakini tuko tofauti na kwa hivyo tuna majukumu tofauti katika ndoa yetu, majukumu yangu ni kuwa msaidizi wake. Mungu alimuumba Adam na alipoona kwamba Adam yuko peke yake, alimuumba Hawa kuwa msaidizi wake.

Je! Hili lilikuwa somo muhimu katika kunibadilisha? Sana, sana. . . Ikiwa tunaweza kujifunza kujitolea kwa mamlaka ambayo Mungu ameweka katika maisha yetu, kwa hiyo tunajifunza kwamba mwili wetu lazima ujitoe kwa Roho wetu. [8]

**Kujichunguza**

Chunguza kile ambacho Bwana amekufunulia juu ya jinsi ambavyo unahitaji kubadilisha katika eneo la utii. Kisha andika maombi ukimwomba Mungu akusaidie kubadilika.

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

_____________________________________________________________

**Uthibitisho ni nini?**

Uthibitisho ni hitaji kuu la ushirika kwa mwanaume. Waefeso inaelezea jinsi utii ulivyo msingi wa uthibitisho na jinsi ambavyo huweza kuwasilisha uthibitisho wa mamlaka kwa mume.

> Wake, watiini waume zenu, kama kwa Bwana. Kwa maana mume ni kichwa cha mke, kama vile Kristo pia ni kichwa cha Kanisa; naye ndiye Mwokozi wa mwili. Kwa hivyo, kama vile Kanisa lilivyo chini ya Kristo, vivyo hivyo wake na watiini waume zao katika kila jambo. . . . Na mke aone kuwa anamheshimu mumewe.
> (Waefeso 5: 22-24, 33)

Kanuni hii ya kibiblia ya uthibitisho wa malaka ya mume inaweza kuonekana kuwa ya zamani na ya kutisha kwa sababu ya mitazamo ya utamaduni wetu wa sasa, ambao unaweza kuliona hili kama wito wa utumwa. Msingi wa kanuni za Mungu ni mtazamo wetu. Maandiko yanasema, "Kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake" (Mathayo 12:34). Utii ni tabia ya moyo, ambao unapaswa kuwa moja ya uthibitisho endelevu wa mamlaka ya mumeo unaonyeshwa kwa jinsi unavyompa kipaumbele, kumtendea na kuzungumza naye.

| |
|---|
| *Faili lenye ukweli*<br>**Thibitisha- Idhinisha mtu/kitu** |

Wanaume hawakuumba uthibitisho huu, Mungu aliumba hali hiyo ili mume aweze kupokea kutoka kwa mkewe. Alimuumba mwanaume na kuacha nafasi hii wazi ili iweza kujazwa na wewe tu. Hii inaweza kufanikiwa tu pale unapojikabidhi kwake; mtumaini Mungu na ukweli huu. Anamwita mumeo kutimiza jukumu la uongozi katika familia na yeyote yule ambaye Mungu atamwita hupokea nguvu ya kufanikiwa. Haijalishi ikiwa yeye si mkamilifu au ikiwa ameshindwa. Mungu hututia mafuta na kutuweka kwa ajili ya majukumu na madhumuni yetu hapa duniani, naye atatuwezesha. Tunapokataa kumwamini Mungu, sisi tupo katika uasi.

Je! Unatazama utendaji wa mumeo kama hali ya heshima yako? Je! Ni lini Mungu amewahi kutazama kwa namna hiyo? Je! Huo ndio msingi ambao unataka Mungu autumie kukutathimini, kutathmini hali ya upendo wake? Ikiwa unachagua kumtazama mumeo kwa macho ya mwili, sio kupitia macho ya Mungu, basi hii ni dhambi na itasababisha shida na kushindwa. Kazi ya Mungu ni mchakato, kwako wewe na kwa mumeo na Mungu anasema heshima yako na ujasiri wako ni muhimu. Mume anahitaji uthibitisho, upendo na msaada wa kimungu kutoka kwa mkewe. Biblia inatupa onyo kali juu ya kuchagua kuishi kwa miili wetu katika uasi.

> Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti, bali nia ya Roho ni uzima na amani. Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya
> Mungu kwa maana haitii sheria ya Mungu, na wala haiwezi kutii. (Warumi 8: 6-8 )

**Uongozi Sahihi**

Waume, lazima mtamani kujifunza jinsi ya kuongoza, bila kujali ni ngumu kiasi gani au haikuwezekana kiasi gani hapo mwanzo. Tenga wakati wa kujifunza jinsi ya kuongoza kwa njia ya Mungu. Lazima uamini kuwa mke wako ni zawadi kutoka kwa Mungu, ili kukusaidia na kukutia moyo kuwa kiongozi wa kimungu. Ikiwa tabia yake haipo katika viwango hivyo,

usiruhusu hiyo ikuzuie kuongoza kwa upole na kwa upendo, wewe ongoza kama kichwa cha familia. Ishi kwa imani kwamba Mungu anaweza na atampa mke wako shauku na nguvu ya kujifunza jinsi ya kushirikiana na wewe. Ikiwa utaonyesha unyenyekevu mbele za Mungu na kukiri kwamba yeye ndiye kiongozi wako, itaongeza ujasiri wa mke wako kwako.

Wanaume wengi hawakuwa na baba aliyekuwa mfano wa uongozi mzuri. Na makanisa hayawafundishi wanandoa jinsi ya kufanya kazi katika majukumu haya. Wanaume wanahitaji kufundishwa katika eneo hili kwani ni moja ya kazi muhimu zaidi tuliyopewa katika maisha haya ya hapa duniani. Ikiwa hatukufundishwa au tumefundishwa kwa maarifa mabaya na mifano mibaya, basi tumeandaliwa vibaya na tutateswa kutokana na matokeo yake.

Kwa kuwa ni wanaume wachache waliofundishwa uongozi wa kimungu na baba zao, tunahitaji wanaume wengine kuja karibu nasi na kutumia muda kutusaidia kutumia kile tunachojifunza. Mafunzo haya yanaitwa *uanafunzi*, na tunajua yanafanya kazi kwa sababu Yesu anautumia mchakato huu. Hii inaweza kuonekana kuwa ya kutisha, hata ya kigeni, kwa mtu mwingine kujua mambo yetu ya binafsi; lakini Mungu hutumia waamini kutia moyo wengine, kuwaunga mkono, kuwajenga na kuwekeza wao.

Wanaume, katika somo hili mnajifunza jinsi ya kuwatendea mke na familia kama mume na kiongozi. Unapotumia kanuni hizi katika ndoa yako, Mungu pia atawaleta wanaume maishani mwako ambao wanahitaji kufundishwa katika mambo ambayo umejifunza. Kuwa katika maombi juu ya hili.

**CHIMBA ZAIDI**

Je! Unaweza kuona jinsi Maandiko haya yanavyotumika katika kuwafundisha wengine? Wanaume, hii ni pamoja na mke wako na watoto. Eleza kile Mungu anakutaka ufanye, na utekeleze kwa familia yako.

> Basi farijianeni na kujengana kila mtu na mwenzake, vilevile kama mnavyofanya. (1 Wathesalonike 5:11)

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
__________________________________________________________

> Neno la Kristo likae kwa wingi ndani yenu kwa katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa Zaburi. (Wakolosai 3:16)

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
__________________________________________________________

> Mchukuliane mizigo na kuitimiza hiyo sheria ya Kristo. (Wagalatia 6: 2)

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

__________________________________________________________________

_______________________________________________________

Pengine umefanya makosa makubwa na unafikiria uko mbali sana na kile ambacho Mungu amekuita ufanye; hiyo bado ni sawa. Jambo kuu juu ya Mungu ni kwamba, bila kujali ni nini kimetokea au ulipoanza, bado unaweza kubadilika. Jitolee kujifunza; weka ahadi ya kuwa mume au mke aliyekuita uwe. Utabarikiwa ukifanya kwa njia yake.

Waume, hatuna thamani ya asili ya upendo na kipaumbele ambacho Mungu huwaambia wake zetu watupe. Lakini Baba yetu wa mbinguni aliye na upendo aliweka uhitaji huu ndani yetu, aliwaita wake zetu na kuwaumba ili waujaze ndani yetu. Na wanapochagua kufanya hivyo, Mungu huwapa neema na uwezo wa kufanya hivyo. Tumsifu Yesu!

> Apataye mke apata kitu chema,
> Na ajipatia kibali kwa Bwana. (Mithali 18:22)

Wanaume wengine hupokea kibali kikubwa kutoka kwa Mungu kupitia wake zao. Lakini kuna wake ambao huleta makosa ya zamani na kuonyesha kila wakati kuwa mume wao hafanyi vizuri.

> Kutona tona daima siku ya mvua nyingi
> Na mwanamke mgomvi ni sawasawa. (Mithali 27:15 HCSB)

Wanawake, *kubughudhi* kunamaanisha kuwa mtu mwenye ugomvi na mke mwenye ugomvi hawezi kumtegemea
Bwana na kumtii. Ni kinyume cha kudhibitisha na mtazamo huu hautatimiza mapenzi ya Mungu maishani mwako. Kile ambacho mwanaume anahitaji ni mke ambaye anaamini kwamba Mungu amemwita aongoze na kwamba Mungu atampa kila kitu kinachohitajika kukifanya; huu pia ni mchakato. Tunapopitia mchakato wa Mungu kwa upendo na uvumilivu, tunapata kuonyeshana jinsi amabvyo tunaweza kukua na kubadilika. Huyu ni mjenga imani na anatutia moyo tunapomwona Mungu akifanya kazi katika maisha yetu.

**CHIMBA ZAIDI**
Andika sala kila baada ya Andiko, kumuomba Mungu atimize kile kinachosemwa, kwanza katika maisha yako na kisha ya mwenzi wako.

> Lakini kuweni katika neema na katika kumjua Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo. Kwake uwe utukufu sasa na milele. Amina. (2 Petro 3:18)

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

_______________________________________________________

> Ndugu imetupasa kumshukuru Mungu kila wakati kwa ajili yenu, ndugu, kama ilivyo wajibu, kwa kuwa imani yenu inakua sana, na upendo wa kila mmoja wenu umezidi kila mmoja kwa mwenzake. (2 Wathesalonike 1: 3)

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

## Somo la 5

## Matendo ya Kawaida ya yasiothibitisha Mamlaka

Tumejadili juu ya uthibitishaji wa mamlaka, lakini inakuwaje pale ambapo mke anakuwa hamthibitishi mumewe? Tunajua kwamba *kuthibitisha* ni kuafiki, kukubali na kuwa na imani kwake kwa kumuonyesha heshima katika matendo na maneno yako na kwa kutii maamuzi yake pale inapohitajika. Tutazame tofauti kati ya kuthibitisha mamlaka na kutokuthibitisha.

### Je! Hii Inajenga?

Wanawake, je, mnalalamika kwa marafiki au ndugu juu ya kushindwa kwa mumeo? Mume wako anaweza asisikie kile unachosema, lakini Bwana husikia. Usijaribu kuifanya iwe ya kiroho kwa kusema, "Ndiyo, huyu ni rafiki yangu wa karibu na mwenzangu katika maombi." Unaweza kusema, "Mimi na mume wangu tunahitaji maombi," badala ya kuelezea makosa yake. Kulalamika juu ya mumeo ni kutomtii Mungu na kutakuwa na madhara yake. Hakuna kinachofanyika kwa siri (Waebrania 4:13).

### CHIMBA ZAIDI

Tambua kile ambacho Maandiko haya yanatuamuru kufanya kuhusu mazungumzo yetu.

> Neno lo lote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema lenye kumfaa muhitaji ili liwape neema wanaostahili. (Waefeso 4:29)

_______________________________________________________________
_______________________________________________________________
_______________________________________________________________
_______________________________________________________________
_____________________________________________________

> Kuna anenaye bila kufikiri, kama kuchomwa kwa upanga;
> Bali ulimi wa mwenye hekima ni afya. (Mithali 12:18)

_______________________________________________________________
_______________________________________________________________
_______________________________________________________________
_______________________________________________________________
_____________________________________________________

> Ulimi safi ni mti wa uzima,
> Bali ukorofi wa ulimi huvunja moyo. (Mithali 15: 4)

_______________________________________________________________
_______________________________________________________________
_______________________________________________________________
_______________________________________________________________
_____________________________________________________

> Maneno ya kinywa changu na mawazo ya moyo wangu yapate kibali mbele zako Ee Bwana,
> Mwamba wangu na Mkombozi wangu. (Zaburi 19:14)

________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
__

> Yeye alindaye kinywa chake huhifadhi nafsi yake;
> Bali afunuaye midomo yake atapata uharibifu (Mithali 13: 3)

________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
____________________________________________________________

**Kuwa Msaidizi**

Mke anapomsahihisha mumewe mbele ya watu wengine, wakiwemo watoto, anakuwa haionyeshi kuthibitisha mamlaka yake na umoja katika kusaidiana. Ikiwa haukubaliani juu ya hali ya malezi, jadili naye kwa faragha. Haupaswi kumsahihisha mumeo mbele ya watoto isipokuwa la sivyo utakuwa unampinga Mungu na mpango wake. Wanawake, ikiwa unafanya hivi, hupati furaha na amani ambayo Mungu anataka uwe nayo kwa sababu haimthibitishii mumeo. Ndio, anahitaji ushauri wako, lakini zingatia maneno yako kwa uangalifu. Vivyo hivyo, wanaume, wake zetu ni zawadi kutoka kwa Mungu kwa sababu wanatukamilisha, na hiyo inamaanisha tunapaswa kuzingatia wanachosema.

Kumhimiza mume wako abadilike katika hali ya uzazi inaweza kumaanisha kumchukua mumeo kando na kuuliza ni kwanini alikuwa akimfokea mwanao. Kisha ukimkumbusha kwa neema kwamba kupiga kelele hakusaidii na kupendekeza nidhamu inayofaa badala yake. Anahitaji ushawishi wako wenye kutia moyo. Una ufahamu juu ya roho za watoto wako ambazo yeye hana. Ni zawadi. Itumie ipasavyo kulingana na njia za Mungu. Uamuzi ni wako. Mke anayeunga mkono atakuwa na mtazamo kulingana na Maandiko haya.

> Na ndugu yako akikukosa, enenda ukamuonye, wewe na yeye peke yenu. Akikusikia, umempata ndugu yako. (Mathayo 18:15)

Hii inahusiana na busara, kuweka faragha katika chochote kilichotokea na kukishughulikia bila ushiriki wa mtu mwingine. Huo ni upendo na tunapaswa "kuusema ukweli kwa upendo" (Waefeso 4:15).

**Mtu wa Matengenezo ni Nani?**

Wake, sio heshima wala utii kwa mume kutendewa kama fundi au mtumishi wa nyumbani. Kuendesha nyumba ni suala la ushirika, haswa ikiwa una watoto wenye nguvu . Wakati mumeo anaingia kutoka kazini, je, unayo orodha ya vitu vya yeye kufanya?

Ikiwa una watoto wenye nguvu wanaoishi nyumbani, kuwapa kazi za nyumbani sio tu inasaidia wao kujua, bali pia inawafundisha uwajibikaji na kujidhibiti; ambayo ni sifa muhimu kwa mtu mzima. Ni kawaida kwa kina mama kuamini kuwa wao wanajali zaidi furaha ya watoto wao, wakati kina baba mara pia hujitahidi katika eneo hili. Watoto wanapoambiwa kufanya kazi na wanatoa visingizio, kunung'unika, au kulalamika; wanahitaji mkono wenye nguvu. Usipuuze nidhamu, au ushawishi wa baba katika nyakati hizi. Ni kweli wanawake wanalea, ingawa wakati mwingine wanafanya makosa; wakati

mwingine wanapoona takataka zimejaa jikoni, badala ya kumwambia mtoto wao wa miaka kumi na miwili akazitoe, wanasubiri hadi baba arudi nyumbani wanamwambia yeye ndo afanye kazi hiyo. Wanawake wanahitaji kulinda mioyo yao katika eneo hili na kuomba kwa Mungu awasaidie kutanguliza mamlaka na mahitaji ya waume zao.

**Je! Hii ni Kuonyesha Heshima?**

Shirikiana na mumeo katika kuweka sheria na kuwaadabisha watoto; maana hii ni njia ya kumthibitisha, na wala usidharau neno lake au mamlaka yake kwa watoto. Je! Unamdhalilisha mbele ya watoto au nyuma ya mgongo wake? Ikiwa mumeo atatoa adhabu (utake au usitake), usimdharau kwa kusema, "Ah, unajua baba yako; atasahau baada ya siku kadhaa, "na unaacha mtoto wako asizingatie nidhamu, hiyo sio kuthibitisha mamlaka yake na wala sio kuwa msaidizi mzuri. Watoto wataanza kukutumia katika udanganyifu na kumpa mzazi mmoja kipaumbele dhidi ya mwingine.

Wazazi wengi hawajafunzwa katika kua walezi. Tafadhali angalia Malezi ni Mfululizo wa Huduma huko FDM.world ili kupata ufafanuzi kamili wa sheria, madhara, kazi za nyumbani na jinsi ya kutekeleza nidhamu ya kimungu. Kimeandaliwa kukidhi rika zote na kila aina ya familia.

Wanawake, je! Unatambua kwamba utapoteza heshima kwa mumeo ikiwa hakukusahihisha kwa upendo wakati ambapo unakuwa huthibitishi mamlaka yake? Unaweza kupata hasira, lakini unatakiwa kutii ikiwa atakuambia, "Nimesikia ulichosema, huna haja ya kurudia; au sitahitaji uniambie jinsi ya kuendesha gari." Kusema chochote zaidi katika hali kama hiyo ni kuanzisha mawasiliano yasiyothibitisha mamlaka yake. Chagua kumthibitisha na ujifunze kutoka katika kila hali. Wanaume wengi wako tayari kufanyia kazi maoni yenye busara, kuliko kupambana na tabia zako.

**Je! Unachagua Kuteseka au Kutumikia?**

Matatizo huibuka wakati mke ambapo, mke ama kwa ujinga, ukaidi, au kiburi, anakuwa hayuko tayari kumtumikia mumewe. Ikiwa huyu ni wewe, unafikiri wengine watakuona dhaifu? Au ni suala wa haki? *Naam, mimi pia hufanya kazi, kwa hivyo kwa nini lazima nimhudumie? Kwa nini nimtolee sahani yake? Anahitaji kutoa sahani yake mwenyewe! Na kwa nini nimpe chakula? Anaweza kufuata chakula! Ana miguu miwili.* Wanawake wengi wameathiriwa na falsafa ya kishetani ya usawa, ambayo inamaanisha kutomtumikia mumeo kwa chochote kwa kuwa anachoweza kujifanyia mwenyewe.

Wakati wowote tunapokataa kuwatumikia wengine, hatumuwakilishi Kristo na uhusiano wetu utapata changamoto. Hii haimaanishi mke anapaswa kuchukuliwa kama mtumishi kwa mumewe la, mke ni mtoto wa Mungu pia na ni zawadi kutoka kwake, hivyo anapaswa kuchukuliwa kama zawadi ya thamani.

**Kujichunguza**

Je! Unatafuta njia za kumtumikia mumeo, iwe nyumbani au hadharani?

___ Ndio ___Hapana

Bainisha namna nne ambazo unazoweza kumtumikia mumeo na uzilete mbele za Bwana kila siku kwa maombi. Muulize maoni yake ikiwa hauna uhakika na jambo hilo.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________

**CHIMBA ZAIDI**

Paulo na wenzake waliwahudumia watu kila wakati. Kusudi lao lilikuwa nini na mtazamo wao ulikuwa nini kuelekea kuwatumikia wengine?

> Bali tulikuwa wapole katikati yenu, kama vile mlezi awatunzavyo watoto wake mwenyewe. Vivyo hivyo nasi tukiwatumaini kwa upendo mwingi, tuliona furaha kuwapa; si Injili ya Mung tu bali na roho zetu pia kwa sababu mmekuwa wapendwa wetu. (1 Wathesalonike 2: 7-8)

________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
____________________________________________________________

Mungu amekupa zawadi ya kuwa msaidizi wa mumeo. Je! Unapaswa kutumia vipi zawadi yako, na kwa nini?

> Kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu. (1 Petro 4:10)

________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
____________________________________________________________

**Je! Uchumi ni Kikwazo?**

Kutakuwa na nyakati ambazo hamtakubaliana juu ya masuala ya kiuchumi. Wake, ikiwa haukubaliani na mgao wa fedha, eleza ombi lako kwa unyenyekevu au toa maoni yako kwa adabu, kisha umwachie Bwana katika maombi kwa ajili ya mumeo. Hata ikiwa mume wako anakiuka maagizo ya Maandiko katika eneo hili, karipia njia zake kwa busara, ukihusisha na hali yake ya kiroho; na siyo kwa uchungu, hasira, malalamiko, kumpuuza na tabia nyingine kama hizo.

Pesa ndio sababu ya kwanza ya talaka, lakini Mungu hairuhusu talaka kwa sababu ya shida za kifedha. Mara nyingi sana wake huruhusu mabishano na mijadala baada ya kutoa maoni yao, ambayo huweza kuwa, "Sikuamini." Labda amestahili kutokuaminika, lakini kumbuka Mungu yuko kazini. Mungu hutubadilisha kupitia hali ngumu na hali hii pia inamstahili

Mungu. Ikiwa hali hiyo inahusisha udanganyifu, uraibu, au ukosefu wa uwajibikaji kwa familia, hii ndio nafasi ya kupata maoni ya kitaalam au ya kichungaji.

**Je! Upendo Wako ni Uwanja wa Vita?**

Kuna mapambano mengi juu ya mahitaji ya ushirika katika eneo la tendo la ndoa. Mke ambaye hayuko tayari kufanyia kazi uhusiano wa kimwili, ambao unaweza kuhitaji kuzoea mahitaji ya mumewe, anakaribisha matatizo. Tendo la ndoa ni mojawapo ya njia muhimu ambayo mamlaka ya mwanaume huweza kuthibitishwa. Mke anayetumia mojawapo ya kauli zifuatazo yuko katika dhambi: *Ikiwa ninahisi umetenda kama mume na baba mzuri, labda nitakupa zawadi. Hustahili hii, lakini nitafanya tu basi. Sawa, acha tu tukamalize hili*. Hii yote ni mifano hasi na ya kudhalilisha, tabia isiyo ya uthibitisho wa mamlaka ya mume.

Picha za ngono zimekuwa ni athari ya kawaida kwa wanaume. Je, ni makosa na ni dhambi? Ndio. Lakini mumeo atakuwa muathirika zaidi ikiwa utakuwa unamkatalia ndani ya ndoa. Mungu aliwaumba wanaume kupata uthibitisho muhimu na kutimilizika wanapokuwa karibu na wake zao. Ni kweli, picha za ngono ni mbadala mbaya kwa kuwa zinaharibu makusudi ya Mungu. Lakini mke anayemzuilia mumewe kwa sababu binafsi pia ni mbaya. Unapojitoa kwa hiari yako kimwili, unambariki mume wako kwa kumthibitisha kwa njia muhimu zaidi.

Wanaume, tuwe wavumilivu. Mungu katika mpango wake kamilifu, anajua majira yote ya maisha ambayo mwanamke hupitia. Wana mizunguko ya homoni ya kila mwezi, watoto, kuongezeka uzito, mabadiliko ya mwili, matatizo ya kike, na hata wakati wa kukoma hedhi; yote Mungu aliyaweka kwa kusudi. Ni muhimu sana kwetu kama waume wazuri kuwa wavumilivu. Mara nyingi waume hukata tamaa, huacha kujaribu na hukaa mbali na uhusiano wao wa mwili ambao Mungu anataka uwepo. Kuna jaribu ambalo kuchukuliwa kama linakubalika, kwa kutafuta kujifurahisha mwenyewe kwa sababu ya kutotimiziwa mahitaji yao ya kimwili katika uhusiano wa ndoa. Baada ya miaka kumi hadi kumi na tano ya ndoa, wanandoa wengi huwa na uhusiano mbaya wa kimwili, mbali na kile ambacho Mungu aliiumba kiwe.

Wanawake, kwa uwianao wa 1 hadi 10, ni jinsi gani uhusiano wa kimwili na mumeo ni muhimu kwako? Pengine mumeo yuko katika uwiano wa 12? Mungu ndiye kamuumba hivyo. Je! Mumeo angeweza kusema uhusiano wako wa kimwili ni muhimu kiasi gani kwako? Ingawa wapo wake wachache wanaweza kuwa karibu na uwiano wa 10, wanaume wengi wangesema 2, 3, au 4. Lakini Mungu aliumba hayo yote kwa makusudi. Tofauti hizi zipo kwa kusudi fulani: pengine ili kujifunza maana ya kujitolea, kujikana wenyewe na kushirikiana ili kutimiza mahitaji ya kila mmoja.

Wanandoa wanapokwenda kwenye ushauri na saha, kwa sababu mume amekamatwa akiangalia picha za ngono, mke hukasirika na mume huwa na aibu. Mara nyingi mume huelezea kuwa wanakutana kimwili mara moja kila baada ya miezi mitatu na imekuwa hivyo kwa miaka mingi. Anajua ni mara nyingi kiasi gani mume angependa kufanya tendo la ndoa, lakini bado anamlaumu kwa chaguo lake la dhambi huku akiwa hayuko tayari kubeba lawama za matendo yake mwenyewe.

Alichokifanya kilikuwa kibaya yaani, *dhambi* — lakini inaeleweka kwa sababu alimtazama mkewe kwa miaka kadhaa na alikataliwa kwa asilimia 98 ya wakati wote aliomuhitaji? Vitendo vya mke vinaonyesha kutokuthibitisha mamlaka yake kwa kumwambia kuwa hitaji lake ni la ubinafsi. Picha za ngono ni mbaya na hazifai kabisa, lakini Wakristo wanaogopa kuzungumza juu ya suala la tendo la ndoa ili waweze kupata msaada wakati wanapokuwa

na changamoto. Mungu ndiye alibuni tendo la ndoa na kwa asilimia 100 ni maalum kwa watu walioowana.

Wanandoa wengi hawapati utimilifu wa ki Mungu uliopo. Tendo la ndoa ni nzuri na linakidhi mahitaji ya kimwili na ya kihisia yaliyojengwa ndani yetu kama wanadamu. Ni hitaji la ushirika kwa *wote* mume na mke. Wakorintho wa Kwanza 7: 4 inafundisha kwamba mke hana amri juu ya mwili wake bali mumewe; vivyo hivyo mume hana amri juu ya mwili wake bali mkewe, ni lazima tuzingatie mahitaji na matakwa ya kila mmoja.

> Msinyimane, isipokuwa mmepatana kwa muda ili mpate faragha kwa kusali; mkajiane tena, Shetani asije akawajaribu kwa kutokuwa na kiasi kwenu (1 Wakorintho 7: 5)

Waume, ikiwa mmekua mmepotoka au mmegeukia dhambi kwa sababu ya kuchanganyikiwa au kujaribu kufufua ndoa yenu kwa kuomba kwa mkeo kile kinachozuilia kila mara, tubu na omba, "Mungu, safisha moyo wangu." Unahitaji kuiondoa akilini mwako dhana hiyo ya dhambi. Ni makosa, ni dhambi na Mungu atakupa neema ya kufunguliwa kutoka kwayo.

Zungumza na mwenzi wako juu ya uhusiano wenu wa kimwili. Jadilini ni nini kizuri na cha kupendeza kwa wote wawili. Kuwa tayari kusikia kutoka kwa kila mmoja na kubadilisha matarajio yako; hii ndiyo maana ya kumpenda mwenzi wako.

Tazama juzuu ya 4, *Utimilifu wa Kimwili*, ili kujifunza kwa kina mada hii.

Sasa nenda kwa Mungu kwa maombi:

> *Baba, nakushukuru na kukusifu wewe kwa ajili ya Neno, kwa kile ambacho linatufunulia. Asante kwa kutupa Roho wako Mtakatifu, nguvu ambayo inatuwezesha kufanya vitu vyote ambavyo unatamani. Baba, ambapo kumekuwa na mgawanyiko, ambapo kumekuwa na ubinafsi, ambapo tumekuwa wakaidi kwa Neno lako, ninaomba kwamba utazungumza na mioyo yetu na kutubadilisha. Tukumbushe yale tuliyojifunza. Tupe hamu ya kusoma, kufuata utakatifu, kujikabidhi kwenye mapenzi yako, kubadilisha vitu ambavyo havikukutukuzi. Bwana, tunakushukuru kwa zawadi ya ndoa na tunaomba kwamba tukutukuze kwa utii katika kila hali ya uhusiano wetu. Tunaomba mambo haya kwa jina la Yesu. Amina.*

**Kwa Maombi Zaidi**

Ili kukusaidia kutumia kanuni ambazo umejifunza, kamilisha *Kiambatisho H: Mahitaji ya Mume* na *Kiambatisho L: Mahitaji ya Ushirika*.

Ikiwa unahitaji msaada ili kuamua nguzo imara ambazo zinakusaidia usitoke kwenye ubora wa Mungu kwa ndoa yako, kamilisha *Kiambatisho M: Vikwazo vya Kawaida* .

# Somo La 6

## Mahitaji ya Wanawake

Sasa tunageukia mahitaji ya ushirika ya mke, ambayo yanaweza tu kutoshelezwa na mumewe anayempenda. Wanaume, lazima mkumbuke kuwa lengo letu ni kuelewa na kutii mapenzi ya Mungu, sio yetu au ya ulimwengu. Kuna mkanganyiko mkubwa juu ya jinsi ya kukidhi mahitaji ya ushirika kwa mke. Vyombo vya habari vimetukanganya na ushauri usio wa kibiblia, usiomcha Mungu na wengi wameukubali. Anza mada hii kwa moyo mkunjufu, ukitaka kusikia kile ambacho Mungu anasema.

Wito wetu ni kuwa wahudumu kwa wenzi wetu na nia yetu ya kufanya hivyo ni kumtukuza Mungu. Unapoendelea mbele, mabadiliko lazima yatokee katika fikra na matendo yako. Kuzingatia Neno la Mungu sio rahisi, kwa hivyo ni muhimu kudumisha msingi imara ambao ni uhusiano wako na Kristo. Tunapokaa na kumtii Kristo, baraka na nguvu zake zinatuwezesha kutimiza mapenzi na makusudi yake.

Neno la Mungu limekamilika na liko wazi katika Waefeso 5 kwamba mume ana jukumu la kutosheleza mahitaji ya mkewe kama vile yeye anavyokutana na yake. Wanaume, mwacheni Mungu akuangazeni juu ya kile ambacho mkeo anahitaji. Wanawake, jifunzeni jinsi Mungu alivyobuni mahitaji fulani ndani yenu ambayo yanaweza kutimizwa tu kupitia uhusiano wako na mumeo. Wote mnapaswa kufuata mpango wa Mungu, ambao ndio unaleta utimilifu, amani na neema yake katika ndoa yako. Nani anajua bora juu ya ndoa kuliko Muumba?

### Mungu Aliumba Mahitaji ya Ushirika

Soma mistari hii mara kadhaa, itowayo mwongozo maalum katika jukumu la mume lililotolewa na Mungu katika yeye kukidhi mahitaji ya mkewe.

> Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama vile Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno, apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na hila wala kunyanzi wala lolote kama hayo, bali liwe takatifu lisilo na mawaa. Vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Ampendaye mkewe ajipenda mwenyewe; maana hakuna mtu aliyechukia mwili wake popote, bali huulisha na kuutunza, kama Kristo naye anavyolitendea Kanisa. Kwa kuwa tu viungo vya mwili wake, "Kwa sababu hii mtu atamwacha baba yake na mama yake na ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja." (Waefeso 5: 25-31)

Ikiwa utachukua maneno haya yote na kuyaweka katika dhana moja, basi dhana hiyo itakuwa *usalama*. Wanaume, natumaini ni dhahiri kwenu kwamba Mungu ana mpango ambao utasababisha mke wako ajihisi salama. Mwanaume anapopenda mkewe kama Kristo alivyolipenda Kanisa lake na akajitolea kwake kuliko wengine wote, yeye hutoa usalama.

| **FAILI LENYE UKWELI** |
|---|
| Ulinzi- usalama, dhamana; uhuru wa kuondokana na hofu. Kutohisi mashaka, hali ya kulindwa isiyo hatari |

Unatimiza jukumu muhimu katika kukidhi mahitaji ya mke wako. David Jeremiah alisema yafuatayo;

> Pindi mume anapompenda mkewe, humpa hali kubwa ya usalama na mume anapompenda mkewe kama Kristo alivyolipenda Kanisa, upendo wa mume

hutoa usalama katika ukaribu kwa kimwili, utambulisho na usalama wa masuala ya kiroho kwa mkewe. [9]

Waume, ushiriki wako katika usalama wa mke wako lazima uwe kipaumbele cha kwanza. Ni ngumu kwetu kuendana na hii. Tuko salama

ndani yetu kwa sababu Mungu ametufanya tuwe viongozi. Lakini Mungu ametuagiza tukae na wake zetu kwa akili na hekima, huku ukimpa
mke heshima kama kiumbe dhaifu" (1 Petro 3: 7). Peter alisema,

waume wanapaswa kuwaelewa na kujali mahitaji ya wake na kutimiza mahitaji yao kiroho, kihisia, na kimwili." [10] *Dhaifu* huwakilisha udhaifu wa kimwili au kihisia na siyo udhaifu wa kiakili. Hii sio kauli hasi, ni namna tu ambayo Mungu amewafanya wanawake kuwa; na waume na wake wanahitaji kuelewa uumbaji huo wa Mungu.

**FAILI LENYE UKWELI**

*Ulinzi*-Hali ya kuwa huru toka kwenye hatari, tishio; kujiamini kuwa mtu ana ulinzi, kwamba maisha ya mtu yanalindwa na mwingine. Kama ilivyo usalama wa mwanamke katika uongozi wa mume.

Uchunguzi wa Waefeso 5 utaonyesha jinsi ambavyo Mungu ameandaa mpango wa kukidhi mahitaji ya usalama wa mke katika ndoa na jinsi mumewe anavyohusika katika kukidhi mahitaji hayo; kwa mpango kamilifu wa Mungu. Mahitaji haya matano yanaendelea pia kupitia somo la 8.

**Hitaji la Kwanza la Mke katika Ushirika**

**Mume anapaswa kumpenda mkewe kama Kristo alivyolipenda Kanisa.**

Mungu anajua kuwa huu ni mpango wake kwamba; mke anapata usalama kwa kupendwa. Anawapa waume maagizo ya wazi: "Wapendeni wake zenu, kama vile Kristo alivyolipenda Kanisa na akajitoa mwenyewe kwa ajili yake" (Waefeso 5:25). Hapa, neno hili *upendo* ( *agape* kwa Kiyunani) ni kitenzi cha wakati uliopo, kitenzi muhimu kinachoonyesha amri ya kufanya na kuendelea kufanya jambo bila kuacha. Dhana hiyo hiyo iliwasilishwa katika juzuu ya 1, tulipojifunza kwamba wenzi wote wawili wanao uhitaji wa upendo wa kishirika; na sasa tunazungumza na waume juu ya kuwapenda wake zao.

**FAILI LA UKWELI**

*Upendo*-mwitiko wa moyo wa Mungu kwa wenye dhambi wasio na thamani; upendo wa Mungu unaodhihirika kwa dhabihu binafsi kwa faida ya wengine bila kujali matendo yao." [11] "Inajumuisha Mungu kufanya jambo kwa ajili ikiwa mtu huyo anakitamani au la… kwa mtoto wake kuleta msamaha'' 12, ni upendo usio wa masharti.

Kiwango ambacho mume anapaswa ampenda mkewe kinalinganishwa na upendo wa Yesu kwa Kanisa, kwa ajili yetu.

Je! Ni kwa kiasi gani Yesu alilipenda Kanisa na alithibitishaje? Yesu alithibitisha upendo wake kwetu hata kwa kifo chake.

Tuko salama katika pendo hili kwa kile Yesu alichokifanya msalabani, sio kile tulichofanya sisi au kile unachofanya sasa.

Je! Hapo sio mahali pazuri kuwapo? Na hiki ni kitu muhimu kwa Mungu ambaye hutafuta tunachohitaji sana kuelewa katika vichwa vyetu, wanaume. Mungu anataka umpende mkeo kwa njia hiyo hiyo, *bila masharti* , sio kulingana na utendaji wake.

Yesu anakuamuru umpende mkeo kwa njia ile ile kama yeye apendavyo, ambayo mwishowe ilisababisha kifo chake cha kujitoa dhabihu msalabani. Ni chaguo lake kwa kujitolea msalabani. Tumshukuru Bwana kwamba hatuhitajiki kufa kimwili, badala yake "ni kufa katika kihisia za kibinafsi" ikimaanisha ubinafsi wetu, ukali na mapendeleo yetu binafsi lazima yatoweke. Kupenda kama Kristo alivyolipenda Kanisa inahitaji utii kwa Neno la Mungu, hata wakati ambao tunakuwa hatuhisi upendo. Lazima tutafute nguvu za Mungu kuwapenda wake zetu ipasavyo, sio kwa kile watakachoturudishia sisi au ili kuwadhibiti au kuwaendesha. Yesu alituonyesha mfano wa jinsi tunavyopaswa kupenda.

Yesu alituwekea mfano, jinsi tunavyopaswa kupenda. Pindi mume anapoamua moyoni mwake kufa nafsi yake yaani kuacha kutenda kwa mapenzi yake mwenyewe na kutenda kwa mapenzi ya Mungu na Roho Mtakatifu, basi upendo huu wa Mungu huanza kutiririka kwa mkewe.

**CHIMBA ZAIDI**

Tambua kile ambacho Maandiko haya huwaambia wanaume wafanye na kwanini ni kanuni muhimu katika kumpenda mke wako.

Ninyi waume, wapendeni wake zenu na msiwe na uchungu nao. (Wakolosai 3:19)

________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
____________________________________________________________

Uchungu na ghadhabu na hasira na kelele, na matukano yaondoke kwenu, pamoja na kila namna ya ubaya. (Waefeso 4:31)

________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
_______________________

Eleza aina ya mawazo na nia ambayo unapaswa kuwa nayo wakati wa kumpenda mke wako.

> Mkaenende katika upendo, kama Kristo naye alivyowapenda ninyi tena akajitoa kwa ajili yetu sadaka na dhabihu kwa Mungu kuwa harufu ya manukato. (Waefeso 5:2)

**Kujichunguza**

Sasa kwa kuwa umejifunza matarajio ya Mungu kwenye kumpenda mkeo kutoka katika Maandiko haya, tambua maeneo yoyote yenye changamoto ambayo Bwana amekuletea akilini mwako. Ungama dhambi yako kwa Mungu na ufuate kwa kuomba msamaha kwa mke wako.

**Mabinti**

Mungu ni "Baba" yetu, na wake zetu ni "binti" zake. Nina binti mmoja na ninamtakia mema kabisa. Wakati atakapoamini kuwa amepata mtu huyo maalum kwa ajili yake, nitawekeza muda na nguvu kwa kijana huyo. Nitamjulisha jinsi binti yangu alivyo muhimu na maalum kwangu na nitahakikisha anaelewa nini maana ya kuwa mume na baba. Nitahakikisha kuwa anasikia ukweli wa Mungu na kutumia kila njia ya ushawishi ili kumsaidia kujikabidhi kwake, kwa sababu nampenda sana binti yangu.

Kama mwanaume, lazima utambue kwamba Mungu anamwona mke wako kama binti yake mwenyewe. Yeye anasubiri na yuko tayari kuweka kila kitu unachohitaji ndani yako ili uweze kumpenda mkeo kwa njia yake.

**Shauku na Vitendo ni vya Muhimu**

Ni kwa shauku ya kweli tu ya kumpenda mkeo kwa njia ya Mungu ndipo utaacha matarajio ya ubinafsi na hali ambazo zinaweza kutawala upendo wako kwake. Unapoingia na kudumu zaidi katika upendo, ndipo utaona moyo wako ukibadilika. Katika juzuu ya 2, tuliangalia kwa kipekee sifa za upendo na jinsi tunavyopaswa kupenda wenzi wetu kutoka katika 1 Wakorintho 13: 4-7. Waume, andiko hilo linatoa uwasikilishi wa kibiblia juu ya njia za vitendo za kuonyesha upendo. Lakini lazima usonge mbele ujue jinsi ya kutenda, kujitahidi, kutamani na kufanya kazi kuona upendo huu uliodhihirishwa kwako ndani ya mke wako.

**CHIMBA ZAIDI**

Eleza jinsi kanuni hizi zitavyokusaidia kutamani na kufuata kumpenda mke wako.

Tena tusichoke katika kutenda mema, maana tutavuna kwa wakati wake tusipozimia roho. (Wagalatia 6: 9)

Lakini zikimbie tamaa za ujanani; akafuate haki na imani, upendo na amani pamoja na wale wamwitao Bwana kwa moyo safi. (2 Timotheo 2:22)

Wala hatuachi kuikumbuka kazi yenu ya Imani na taabu yenu ya upendo. (1 Wathesalonike 1: 3)

Upendo na lisiwe la unafiki. (Warumi 12: 9)

Walakini mwisho wa agizo hilo ni upendo utokao katika moyo safi, na dhamiri njema, na imani isiyo na unafki. (1 Timotheo 1: 5)

Bwana na awaongeze na kuwazidisha katika upendo (1 Wathesalonike 3:12)

> Na hii ndiyo dua yangu kwamba pendo lenu lizidi kuwa jingi sana katika hekima na ufahamu wote, mpate kuyakubali yaliyo mema ili mpate kuwa na mioyo safi, bila kosa mpaka siku ya Kristo. (Wafilipi 1: 9-10)

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

____________________________________________________________

Ni kupitia msingi wako imara tu —uhusiano wako na Kristo — ndipo unaweza kumbariki mke wako kwa aina hii ya upendo.

**Usalama ni Kinyume cha Hofu**

Lazima tuwapende wake zetu ili waweze kuishi kwa usalama na bila woga. Kanuni hii ya kibiblia inaonyesha tofauti kati ya hofu na upendo.

> Katika upendo hamna hofu; lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu, kwa maana hofu ina adhabu; na mwenye hofu hakukamilishwa katika upendo. Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza.
> Mtu akisema, "Nampenda Mungu," na anamchukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hajamwona. Na amri hii tumepewa na yeye, ya kwamba yeye ampendaye Mungu ampende na ndugu yake. (1 Yohana 4: 18–21)

> Yohana aliwaambia waamini ambao wanampenda Mungu kweli ya kwamba hawahitaji kuogopa siku ya hukumu.

> Katika hili pendo limekamilishwa kwetu, ili tuwe na ujasiri katika siku ya hukumu. (1 Yohana 4:17)

Ufafanuzi mmoja unasema yafuatayo:

> Upendo unaokua kikamilifu unamhakikishia muumini kwamba yuko sawa na Mungu na itamfanya awe na ujasiri siku ya hukumu. Muumini hatakuwa na matarajio ya kutisha. [13]

Muumini hupata upendo uliokamilika kuhusiana na Mungu. Wana uhakika kamili au usalama, wakiamini kwamba Mungu atawashughulikia. Huwa vivyo hivyo pindi unapompenda mke wako, inajenga imani na usalama kwamba utamfanyia yaliyo bora zaidi sawa sawa na mapenzi ya Mungu.

Wanaume, je! Mnasababisha hofu kwa tabia zenu? Upendo huu mkamilifu ambao Yohana alizungumzia unaweza kuja tu kupitia Kristo. Mungu hakuambii wewe fuata mwongozo wake na upate nguvu ya ndani na uwezo wa kumpenda mke wako kwa namna hii. Anasema kwamba unapowasilisha moyo wako, tamaa zako na utashi wako mwenyewe kwake kwa utii na uaminifu, yeye atakujaza shauku ya kumpenda mke wako na upendo wa Mungu utakuwa unamwagika kutoka kwako kwenda kwake.

Katika maisha haya hakuna mwanaume ambaye atakamilika kabisa katika upendo kwa mkewe. Sisi wanadamu ni kazi inayoendelea, lakini ufunguo ni kuzidi kuendelea.

> Nami niliaminilo ndilo hili, kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu. (Wafilipi 1: 6)

Shetani ana ngome ngumu kwa wanaume wengi. Anatuambia, "Hautabadilika kamwe, hii ni ngumu sana kwako. Mke wako ndiye anasababisha ufanye hivi. Jaribu hili huwezi kulishinda. " Huu ni uwongo kutoka kwa Shetani, endapo utauamini, basi utaanza kukuamuru nini kufanya na nini hutafanya; nini cha kuamini na nini hautaamini. Ikiwa mke wako hajiamini au anaogopa kwa njia yoyote ndani ya ndoa, kwanza jichunguze wewe mwenyewe.

***MPANGO KAZI***

Jadilini sehemu hii kwa pamoja kama mume na mke. Mume, angalia hofu yoyote ambayo mke wako amekushirikisha. Kisha sikiliza kwa upendo bila kutoa visingizio, ujifunze jinsi unavyoweza kumhudumia vizuri. Andika kile ulichojifunza kutoka kwake hapa na uombe msamaha inapohitajika.

_______________________________________________________________________
_______________________________________________________________________
_______________________________________________________________________
_______________________________________________________________________
_________________________________________________________

Wanawake, kumbukeni kuwa mumeo ni kazi inayoendelea. Anapojifunza kukaa ndani ya Kristo kwa kutumia muda katika Neno la Mungu na katika maombi, anajifunza kutoka kwenye majaribu na yuko tayari kuomba msamaha, ataanza kubadilishwa kuwa sura ya Kristo, ambayo ni pamoja na uwezo wake wa kukupenda.

Upendo huu wa *agape hauna* masharti. Mungu anatupenda sana kiasi kwamba alimtuma Mwanawe atufie, wakati bado tulikuwa wenye dhambi (Warumi 5: 8), ili kutuonyesha thamani anayotupatia kila mmoja wetu. Wanaume, tunapaswa kuwapenda wake zetu kwa sababu ya thamani ambayo Mungu ameweka juu yao. Hii sio kwa nguvu zetu bali ni kwa nguvu ya Roho Mtakatifu ambaye anakaa ndani yetu ikiwa tumempokea Yesu kama Bwana na Mwokozi. Hii ndiyo zana yetu ya kupimiwa.

Wanaume, msitumie kipimo kingine chochote pindi mnapopima tabia zenu, ila tu yale ambayo Mungu amesema. Unapokosa kuishi kwa upendo huu ambao Mungu anaelezea, uwe na unyenyekevu na dhamira ya kuukiri kwa Mungu na mke wako. Sifa moja ya kiongozi wa kweli ni unyenyekevu (Matendo 20:19; Tito 3: 2), kuwa tayari kukubali kuwa umekosa na beba jukumu hilo. *Kutubu* kunamaanisha "kubadilisha mwelekeo, kuelekea kwa Mungu na kuomba msamaha." Yeye husamehe (1 Yohana 1: 9).

**Epuka kile Kinachokuja kwa Asili**

Wanaume, kile kinachokuja kiasili huwa kinataka tabia za mkeo ziamue jinsi utakavyomtendea. Je, yeye alifanya kile nilichomtaka afanye?, Nini alichokuwa *anatakiwa* kufanya ? Je! Alitumia wakati wake kwa busara na kukutendea vile unataka kutendewa?

Pindi wengine wanapofanya kile tunachotamani, tunawalipa wanavyostahili kwa upendo wetu, nia njema, au kibali. Lakini huo *sio* upendo. Sifa muhimu ya Mungu kuhusu upendo ni kwamba; hautafuti masilahi ya wengine, wala kujali matendo yao. Warumi 5:10 inasema, "Tulipokuwa maadui tulipatanishwa na Mungu," na ni wema wa Mungu ambao unatuongoza kutubu (Warumi 2: 4).

Shauku na harakati za Mungu ziliongezwa katika upendo wake kwetu, hata wakati ambapo hatukustahili. Yeye hatupendi sisi ili kupata kitu kama malipo, bali yeye hufungua mkono wake wa upendo tena na tena ili kushawishi mioyo yetu kwa ajili ya injili. Vivyo hivyo, tunapaswa kufungua mkono wa upendo huu kwa wake zetu ili waweze kumwona Mungu ndani yetu na kuona upendo wake ukipita kati yetu. Hali hii haiji kama asili.

Mungu anatuangalia (Waebrania 4:13), na tunapaswa kujichunguza wenyewe (1 Wakorintho 11: 31-32). Je! Niliishi kwa mfano wa Mungu, au niliangalia tabia ya mke wangu, kile alichonifanyia au kutonifanyia na kuvitumia kuhalalisha jinsi ninavyomtendea?

Mungu anataka umpende na umthamini mkeo kulingana na thamani yake kwake kama binti yake. Wanaume, unapoanza na aina hii ya upendo, Mungu atakubariki na mke salama ambaye ana uwezekano mkubwa wa kuheshimu uongozi wako. lakini, wakati hafanyi vizuri, unaitwa na Mungu kufuata mwongozo wake, sio wa mke. Huu ni ukweli mgumu.

## Somo la 7

## Zawadi kutoka kwa Mungu

Mke wako ni zawadi kutoka kwa Mungu, lakini yeye si mkamilifu. Kuna nyakati yeye hufanya au kusema vitu ambavyo viinakukasirisha, lakini majibu yako lazima yawe sawa na Neno la Mungu. Ulijitolea kumtumikia mke wako na kumpenda kama Kristo anavyolipenda Kanisa. Tumia muda kila siku na Bwana na wacha Roho wake Mtakatifu akusadikishe wakati unapomuhitaji.

Unapokasirishwa na jinsi anavyokutendea, kumbuka jinsi Mungu anavyokupenda. Je! Ingekuwaje ikiwa nyakati zote ambapo ulitenda dhambi Mungu angepoteza uvumilivu kwako na kukutendea kama unavyostahili? Mungu hajawahi kukutendea kwa masharti na haupaswi kumtendea hivyo mke wako. Wakati Roho Mtakatifu anapokuonyesha haya, tubu mtazamo wako, nenda kwa mke wako na umwombe msamaha; hiyo ni sehemu yako.

Unapokosa msimamo na kuruhusu tabia yake au matarajio yako binafsi kuamuru jinsi unavyomtendea, Mungu anaiona hiyo kuwa ni dhambi na hakuna njia ya kuondokana nayo isipokuwa ungamo na toba. Unapojinyenyekeza, kuomba msamaha na kutumia Neno la Mungu kama sheria yako katika kupenda, utapata mabadiliko katika asili yako na kuwa mfano wa Kristo. Ni kwa utii huu tu ndipo utapata upendo wa kweli wa Mungu unaotiririka kati yako na mke wako.

### Hitaji la Pili la Mke katika Ushirika

**Mume anapaswa kumtakasa mkewe na kumsafisha kwa maji katika Neno.**
Mungu anamwambia kila mume kumtakasa na kumsafisha mkewe kwa maji katika Neno.

> Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama vile Kristo alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake, *ili makusudi* ali*takase* na *kulisafisha* kwa maji katika neno. (Waefeso 5: 25-26, mkazo ni wangu)

Kifungu hiki kinamwambia wazi mume kuwa upendo kwa mkewe lazima uonyeshe sifa za Kristo ambaye, alilipenda sana Kanisa, akajitoa kwa ajili yake. Katika mstari wa 26, neno la kwanza tunaloona ni *kwamba*, ongea kwa kusudi. Kristo alitoa maisha yake kwa ajili ya Kanisa ili kulikomboa, kwa lengo la "kulitakasa" (kutenga kwa ajili ya utakatifu) na "kulisafisha" kwa njia ya maji katika Neno la Mungu. Katika umilele, ni Kristo ndiye hufanya utakaso na kumwosha mke, lakini Mungu pia amemchagua mume kuwajibika katika mchakato huu wa utakaso kupitia uongozi wake, kwa katumia mfano wa Neno la Mungu. Hapa ndipo uoshaji wa maji katika Neno huingia. Mungu amempa kila mume fursa ya kushangaza ya kutumia Neno la Mungu lenye thamani kumhudumia mkewe.

Mwandishi mmoja alisema hivi:

> Wakati watoa maoni hawakubaliani juu ya maana halisi ya mstari huo, "kusafisha kwa maji katika neno" (mstari wa 26), wale wachache ambao hata wanajaribu kuutumia wanaonekana kukubali kwamba matumizi ya mstari huu ni aina fulani ya msaada wa mume katika mchakato wa utakaso unaoendelea wa mkewe. Kama yeye kiongozi wa kiroho, lazima "umtenge" (au umtakase), ukimtakasa kupitia Maandiko; lazima umsaidie, kupitia Neno, kuondoa madoa na makunyanzi yake ya kiroho na kitu kingine chochote

[mstari wa 27] ambacho hakilingani na sura ya Kristo. Njia unayotumia katika kulifanya hii ni kwa kutii na kutumia Neno katika shughuli zako zote ukiwa naye. [14]

Habari hii inahusu hatua, sio kuongea au nia nzuri. Walifua vipi nguo siku zile mwandishi huyu alipoandika maneno haya? Hawakuwa na mashine za kufulia. Walikuwa na kijito na ndoo. Walilazimika kwenda chini kwenye kijito, kutoa nguo nje, kuziweka kwenye miamba na kufua kwa mikono yao. Hiyo ndiyo picha ambayo Mungu anaonyesha. Hii ni kazi ya kukusudia. Mpende mkeo kupitia matendo yako, unachosema na kile unachofanya katika mambo yote. Hii ndio sababu Mungu anasema unahitaji kuwa mwanafunzi wa Neno lake (2 Timotheo 2:15). Tunawezaje kuwaosha wake zetu katika Neno la Mungu ikiwa sisi wenyewe hatuko katika Neno lake na kuishi ukweli wake sisi wenyewe?

**Kujichunguza 1**

Pindi mwanaume anapochukua muda kujifunza kuishi kwa njia ya Mungu na kuzingatia vitu ambavyo Mungu amempa, hali hii ni kuosha mkewe katika Neno la Mungu.

Wanaume, orodhesha maeneo ambayo haujiamini kuwa unamtunza mke wako kulingana na Neno la Mungu (kwa mfano, kama mume, mwandani, mzazi mwenzako, katika fedha, n.k.)

____________________________________________________________________________
____________________________________________________________________________
____________________________________________________________________________
____________________________________________________________________________
_____________________________________________________________

Kisha andika maombi kwa Mungu, ukijitolea kutumia wakati kujifunza mapenzi yake kupitia masomo binafsi au kutafuta mtu wa kukufundisha, kukusaidia kujifunza na kukua.

____________________________________________________________________________
____________________________________________________________________________
____________________________________________________________________________
____________________________________________________________________________
_____________________________________________________________

**Ongoza kwa Mfano**

Kama Mungu alivyowateua wanaume kuwa viongozi nyumbani, hatuwezi kutoa sababu ya tabia isiyomcha Mungu kwa wake zetu au watoto. Mke wako atahisi kutokuwa salama na labda ata kuogopa, hali ambayo ni kinyume cha mapenzi ya Mungu. Wakati Mungu anasema unapaswa kuosha mke wako kwa maji ya Neno, anazungumza na wewe kama kuhani, au kiongozi wa kiroho nyumbani kwako. Je! Unatumia wakati wa ibada kila siku na Bwana? Je! Mke wako anakushuhudia ukiwa katika Neno na maombi?

Msingi wa kuwa na uhusiano na mtu ni kutumia muda pamoja nao. Na zawadi kubwa zaidi tuliyopewa kupitia kifo cha Kristo kwa dhambi zetu ni fursa ya kumfikia moja kwa moja Mungu aliye hai. Anatungojea, anatusikiliza na anazungumza nasi kupitia Roho wake Mtakatifu.

Kama viongozi tunaitwa kuwa mifano. Kutumia wakati kila siku katika Neno na maombi sio tu kuonekana, lakini inakuwa halisi tunapoanza kuishi kulingana na Neno. Mke atahisi

salama atakapoona matokeo, atakapoona mtazamo wako mpya kwake na maisha kwa ujumla. Kwa hivyo, wanaume, hii huanza na sisi.

Ikiwa bado unapambana katika eneo hili, tafadhali pitia juzuu ya 1, somo la 7.

**CHIMBA ZAIDI**

Husianisha Maandiko haya na maisha yako. Je! Unapaswa kuwa na mtazamo na shauku gani kwa Neno la Mungu na kazi yake ya utakaso?

> Naye akajibu akasema, "Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu." (Mathayo 4: 4)

> Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa, yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu. (1 Petro 2: 2)

> Jinsi gani kijana aisafishe njia yake? Kwa kutii
> akilifuata neno lako.
> kwa moyo wangu wote; nimekutafuta
> Usiniache nipotee mbali na maagizo yako! (Zaburi 119: 9-10)

> Unifumbue macho yangu, niyatazame maajabu
> Maajabu yatokayo katika sheria yako. (Zaburi 119: 18)

> Ee Bwana, unifundishe njia ya amri zako,
> nami nitaishika hata mwisho. (Zaburi 119:
> 33)

____________________________________________________________
____________________________________________________________
________________________________________________

> Wana amani nyingi waipendao sheria yako,
> Wala hawana la kuwakwaza. (Zaburi 119: 165)

____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
________________________________________________

**Uongozi wa Kiroho**

Wanaume, hili ni jukumu letu, yaani moja ya majukumu yetu ya kikuhani, kuanzisha sala na wake zetu kila siku. *Anzisha.* Wanaume wengine wanasema ni ngumu kusali mbele ya wake zao. Lakini ilikuwa ngumu pia kuendesha baiskeli mwanzoni, sivyo? Ilikuwa hisia ya kushangaza, isiyo na usawa , labda hata ya kutisha.

Labda hujazoea kuomba kwa sauti. Lakini Mungu anataka uwe kiongozi wa kiroho, uanze kuomba na mke wako na kuanzisha maombi. Inaweza kuwa ngumu mwanzoni; na huenda mke wako hataki kuomba kwa sauti. Inaweza kuchukua wiki, miezi, au hata miaka kabla ya mke kujisikia raha kuomba mbele yako. Lakini sio kazi yako kumshinikiza azoee. Kazi yako ni kukidhi mahitaji ya ushirika ambao Mungu ameweka ndani yake. Tutazungumzia hili zaidi katika juzuu ya 5, *Uongozi wa Kimungu*.

Je! Unajua mke wako anasoma nini, anajifunza nini kutoka kwenye Neno? Umemsaidia kuongeza wakati wa ibada? Sio jukumu la Kanisa au huduma ya wanawake kumuosha mke wako katika Neno. Ni jukumu lako kama mume kumsaidia mke wako, hata kushirikiana naye kila siku katika kutafakari Neno la Mungu.

Je! Unazungumza juu ya mambo ya kiroho? Je! Unamuomba au unasikiliza mapambano na ushindi wake wakati anatafuta kuishi maisha ya kimungu? Je! Unashiriki vitu ambavyo Mungu anakufundisha katika maisha yako ya ibada? Mtie moyo katika masomo yake na uwe unamaanisha. Hakikisha unashiriki kile Mungu anasema na wewe bila kumfanya ajisikie duni.

Tunapokuwa wanafunzi wa Neno la Mungu, tunaweza kwa unyenyekevu na kwa upendo kuwafundisha wake zetu. Na kama makuhani nyumbani, ikiwa tuna watoto, tunapaswa kuwafundisha pia. Wanaume wengi hawajawahi kuwa na mfano wa hii, lakini usiiachie nyuma hii shule ya Kikristo au kikundi cha vijana wa Kanisa. Hizi ni nyongeza nzuri, lakini hazichukui nafasi ya uongozi wako.

Ikiwa unataka kutimiza uhitaji wa ushirika wa mke wako katika eneo hili, kuwekeza wakati wako na bidii katika kuwa mwanafunzi wa kweli wa Kristo ndiyo njia ya kuikamilisha. Sio kawaida kwa mke kuwa ndiye anayefanya kazi na kuwa na wasiwasi juu ya kufika kanisani au kuwa katika somo la Biblia au kuchunga hali ya kiroho ya watoto.

Wanaume mara nyingi hukabiliana na tabia ya kukosa ushirikiano wakati wake zao wanataka uongozi wa kiroho kutoka kwao. Lakini hii ni hitaji lililowekwa ndani ya mke wako na Mungu. Hawakuitaka. Unaweza kufikiria amekuwa akikusumbua kwa miaka. "Mpenzi, kwa nini usisali pamoja na watoto na mimi?" Labda unafikiria unalipa vya kutosha

kuwapeleka shule ya Kikristo. Hii ni makosa, na unamkaidi Kristo. Kuna shauku ndani ya moyo wa mkeo ya wewe kuchukua uongozi wa kiroho (Mwanzo 3:16). Mungu alimweka ndani yake.

Wanawake, unaweza kukosea pia. Mtazamo wako unaweza kusababisha ushawishi mbaya. Kumbuka kumuombea mumeo na kumtia moyo na kumthibitisha, ambayo ni tofauti na kumsumbua, na haina dalili ya hukumu

**Kujichunguza 2**

Pitia orodha ya njia za kumtakasa mke wako katika *Kiambatisho J: Njia za Kibiblia Mume Humtakasa Mkewe,* kimejumuishwa mwishoni mwa kitabu hiki cha kujifunziai. Orodhesha ahadi maalum kwa Bwana juu ya jinsi utakavyotekeleza haya kama majukumu yako ya ukuhani.

________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
_____________________________________________

**Mungu Anaahidi Kusaidia**

Maandiko mengi yanatuhimiza kudumu katika tabia ya kimungu na imani tunapojikuta katika hali ngumu.
Wake, ikiwa umeolewa na mtu asiyeamini au mume katika uasi, kumbuka 1 Petro 3: 1-4 juu ya unyenyekevu. Kuwa na moyo wa subila.

> Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. (Mathayo 11:28)

Mungu anatujua pindi tunapokuwa chini ya mamlaka ya mume ambaye yuko nje ya mapenzi ya Mungu. Anajua yote, na Yeye hutupa maagizo ya kumtumaini Yeye (Mungu) na kujitolea kwa mamlaka ambayo ameweka juu yetu (Warumi 13: 1–4). Maadamu haiitaji utende dhambi, mtegemee yeye na matokeo yake. Wakati mke anarudi kwa Bwana na kusema, "Ninajua nina hitaji hili, lakini ninateseka kwa sababu mume wangu hajibu wito wako," basi Baba yake wa mbinguni mwenye upendo atawatendea Anaahidi kutupatia mahitaji yetu yote. Ishi kwa utii kukidhi mahitaji ya ushirika wa mumeo na Mungu atakubariki kwa njia zisizotarajiwa.

**CHIMBA ZAIDI**

Tambua yale Maandiko ambayo yanasema juu ya jinsi Mungu anavyohusika katika maisha yako na jinsi unavyoweza kumwamini katika ndoa yako.

> Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao Mungu,katika kuwapatia mema; yaani wale walioitwa kwa kusudi Mungu. (Warumi 8:28)

__________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________

> Bwana wetu ni mkuu, na mwingi wa nguvu;
> Akili zake hazina mpaka. (Zaburi 147: 5)

__________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________

> Macho ya Bwana yako kila mahali;
> Yakimchunguza mbaya na mwema. (Mithali 15: 3)

__________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________

> Kwa kuwa macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, na masikio yake husikiliza maombi yao;
> bali uso wa Bwana ni juu ya watenda mabaya. (1 Petro 3:12)

__________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________

> Na ndani yake sisi nasi tulifanywa urithi, huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi la yeye ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake. (Waefeso 1:11)

__________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________

> Na Mungu wangu atawajazeni kile mnachohitaji kwa kadiri  ya utajiri wake katika utukufu ndani ya Kristo Yesu. (Wafilipi 4:19)

___________________________________________________________________________
___________________________________________________________________________
___________________________________________________________________________
___________________________________________________________________________
____________________________________________________________

Eleza jinsi tunavyostahimili au kuwa imara katika hali ngumu.

> Kwa sababu hii nimepatikana na mateso haya; wala sitahayari maana namjua yeye niliyemwamini na ninasadiki ya kwamba aweza kukilinda kile nilichokiweka amana kwake hata siku ile (2 Timotheo 1:12)

___________________________________________________________________________
___________________________________________________________________________
___________________________________________________________________________
___________________________________________________________________________
____________________________________________________________

> Hata na sisi wenyewe twaona fahari juu yenu katika makanisa ya Mungu kwa ajili ya sabuli yenu na imani mlionayo katika adha zenu zote na dhiki mnazostahimili. (2 Wathesalonike 1: 4)

___________________________________________________________________________
___________________________________________________________________________
___________________________________________________________________________
___________________________________________________________________________
____________________________________________________________

Tafakari ahadi za Mungu za kukutia moyo wakati wa changamoto zako.

## Somo la 8

## Kumthamini Mkeo

Mahitaji mawili ya mwanzo ya ushirika kwa mke yalijadiliwa katika masomo yaliyotangulia: mpende mkeo kama Kristo alivyolipenda Kanisa na mtakase na msafishe kwa maji katika Neno. Katika somo hili, tunatambulisha hitaji la tatu lililosalia.

**Hitaji la Tatu la Mke katika Ushirika**

**Mume hapaswi kukaa kinyume na mapenzi kamili ya Mungu.**

Mungu, kwa hekima yake isiyo na kikomo, anatupa changamoto kama waume kutokukaa katika kiwango cha chini kwenye ndoa zetu.

> Apate kujipatia Kanisa tukufu lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa. (Waefeso 5:27)

Mstari huu haufunui tu moja ya mahitaji ya kipekee ya ushirika kwa mke, lakini pia unawahimiza wanaume kupambana na wasiwe wavivu au walalahoi katika uhusiano wa ndoa zao. Wanaume wengi wako katika uhusiano wa kimapenzi na wake zao bila hata kujua mapenzi ya Mungu na viwango vya ndoa inayomcha Mungu, badala yake hutumia tu mitazamo yao finyu ya kiume kama kipimo. Wengine hugundua kuwa mambo sio sawa, lakini hawafanyi chochote kurekebisha.

Mke anakuona unapata muda wa kujiendeleza katika kazi yako, kuboresha mchezo wako wa gofu, kusaidia wengine wanaohitaji, au kuhudumu kanisani — lakini sio kurekebisha ndoa yako. Hii ni kinyume na kile Mungu anachosema katika mstari wa 27 hapo juu, ambapo anawahimiza wanaume wasikubaliane na chochote kilicho kinyume na mapenzi yake kamili kwa ndoa zao.

Mungu anajitumia mwenyewe kama mfano wa kuigwa katika Waefeso 5:25, akisema, "Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama vile Kristo pia alivyolipenda Kanisa na akajitoa mwenyewe kwa ajili yake." Kwa kufanya hivyo, anadhihirisha umuhimu na kipaumbele ambacho mume anapaswa kuweka kwenye uhusiano wake na mkewe.

**Kujichunguza 1**

Omba Mungu akupe kutenda kwa moyo wake kwa ajili ya mke wako. Muombe neema ya kujituma na ufanyie kazi kanuni hizi unazojifunza juu ya kumtunza mke wako na kukidhi mahitaji yake ya ushirika. Kwa kutumia nafasi iliyo hapo chini, fanya leo mwanzo wa kujitolea kwako kufanya kazi hii mpaka Mungu atapokuchukua uwe pamoja naye mbinguni.

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

______________________________________________________________________

____________________________________________

**Hitaji la Nne la Mke kwa Ushirika**

**Mume lazima ampende mkewe kama mwili wake mwenyewe.**

Biblia inaendelea kusisitiza na kufafanua jukumu la mume kumpenda mke wake kwa kujitolea kwa kulinganisha na anavyojipenda yeye mwenyewe.

> Vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe; ampendaye mkewe ajipenda mwenyewe. Kwa maana hakuna mtu anayechukia mwili wake popote, bali huulisha na kuutunza, kama vile Kristo naye anavyolitendea Kanisa. Kwa kuwa tu viungo vya mwili wake. (Waefeso 5: 28-30)

Wanaume, hii inasema tunapaswa kuwatendea wake zetu kama ilivyo kwa miili yetu wenyewe. Hii ni ngumu na inaweza kusikika kuwa ya kushangaza kidogo. Je! Umewahi kweli kusikia jinsi mke wako anavyongea na wanawake wengine? Wao ni tofauti na sisi, lakini tunaitwa kuwachukulia kama tunavyojichukulia sisi wenyewe. Wanawake huangalia maisha kwa mtazamo tofauti kabisa na wanaume.

Mungu anataka umpende mke wako kama ilivyo kwa mwili wako mwenyewe, ingawa hii inaweza kuwa ngumu kuelezea. Hatahivyo, inaweza kuhusishwa na dhana ya kutaka heshima na sio kukosolewa au kuwekwa chini kwa jinsi ulivyo. Unaweza kuhusisha kutaka mapambano na hisia zako zichukuliwe kuwa za busara na muhimu. Na unaweza kuhusishwa na kutaka kupendwa na kueleweka.

Jamani, tunahitaji mazoezi mengi. Je! Umewahi kugundua jinsi hisia za mke wako zinavyoumia juu ya kitu unachofikiria ni ujinga? Au yeye huwa na hisia au machungu juu ya kitu ambacho mmoja wa watoto wenu amefanya wakati wewe huhisi hisia yoyote kabisa? Katika hali nyingine, unaweza kuhisi kumwambia aangalie ukweli na ashughulikie. Lakini unajua hatuwezi kufanya hivyo. Mungu ametufanya sisi wanaume kuwa tofauti sana, lakini anasema, "Ingawa wewe ni tofauti sana, nataka ujifunze jinsi ya kumtunza na kumlea kama mwili wako mwenyewe."

Tukio la kusisimua kwako ni kujaribu kumuelewa mke wako. Wanaume, lazima muwaangalie wake na kuwaacha kama walivyo, ila pia muwe na mtazamo mzuri juu yao. Yeye ndiye mke ambaye Mungu alikupa na unahitaji kujifunza jinsi ya kumthamini na kumlea kama ziada ya mwili wako mwenyewe, ingawa yeye ni tofauti sana na wewe. Ingawa hii yaweza kuwa changamoto na jambo la kusisimua, lakini baraka ni kuwa na mke anayeridhika na mwenye furaha.

Kuelezea maana ya maandishi haya katika Waefeso na wazo la mke wako kuwa kama mwili wako mwenyewe, ufafanuzi mmoja unaiweka hivi:

> Kristo anapenda Kanisa, sio tu kana kwamba ni mwili wake, lakini kwa sababu kwa hakika ni mwili wake. Kwa hiyo waume wanapaswa kuwapenda wake zao, si kama vile wapendavyo miili yao wenyewe, bali kama kuwa mwili mmoja na wao, kwa kuwa ndivyo walivyo. Isijekuwa maana nzuri ya kile alichokithibitisha ikakosa kutunzwa na wasomaji wake, Paul anaiweka kwa njia nyingine ili kuepusha utata.

> Uhusiano wa kimwili kati ya mwanaume na mke ni wa karibu sana kana kwamba wameungana kuwa kitu kimoja. Kwa mwanaume kumpenda mkewe ni kujipenda mwenyewe. Hapaswi kuchukuliwa kama kipande cha mali, kama ilivyokuwa kawaida katika siku za Paulo. Anapaswa kuzingatiwa vizuri kama sehemu ya mtu mwenyewe. [15]

Je! Umewahi kugonga kidole gumba wakati wa kupigilia msumari au kubamiza kidole kwenye droo? Je! Ulikusudia kufanya hivyo? Je! Mkono wa kushoto ulijaribu kunyakua nyundo kutoka mkono wa kulia na kuitupa kuzunguka mwili wako ikijaribu kupambana? Hapana. Nyundo ilipogonga kidole chako, mwili wako wote ulifanya kazi kwa umoja kabisa kwa upole na wepesi katika kurekebisha na kuuponya. Hivi ndivyo Mungu anatuita tuwafanyie wake zetu: tuwatendee kama sisi tunavyofanya miili yetu wenyewe. Haijalishi ikiwa anakasirika au amechanganyikiwa na wewe au unafikiri alileta hali hiyo juu yake mwenyewe. Umeitwa kumtendea mke wako kwa upole na uangalifu.

Wakati mke wako anapokwambia jinsi mtu alivyoumiza hisia zake, unaweza kushawishiwa kumkatiza na kumwambia jinsi ya kurekebisha. Lakini mara nyingi anahitaji tu usikilize, hali ambayo ni ngumu kwa mwanaume. Anataka tu kupooza moyo wake na unahitaji kujifunza jinsi ya kumhudumia, sio kama mwanaume, sio kama wewe utakavyo, bali kama jinsi atakavyo yeye. Mke wako ni wa kipekee na Mungu anataka umjue, ndani na nje, ili uweze kumchukulia mahitaji yake na kumchukulia kama sehemu ya mwili wako mwenyewe. Hii inashangaza na inahitaji uvumilivu na bidii, lakini itakupa faida na thawabu kubwa wakati ambapo mke wako anapohisi kuwa anaweza kukuamini kwenye hisia zake. *Hii* ni usalama kwa mwanamke.

**Kujichunguza 2**

Wanaume, fikiria jinsi ambavyo umekuwa ukimtendea mke wako. Tambua angalau njia mbili unazomtendea ambazo usingefanya kwa mwili wako mwenyewe. Kisha nenda kwa Bwana kwa maombi ili ubadilike.

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
__________________________________________

**Hitaji la Tano la Mke katika Ushirika**

**Mume anapaswa kumlisha na kumtunza mke wake.**

Mungu hutumia maneno *kulisha* na *kutunza* anapotuelekeza juu ya jinsi ya kuwatendea na kuwapenda wake zetu. Anasema, "Hakuna mtu aliyeweza kuchukia mwili wake mwenyewe, lakini huulisha na kuutunza" (Waefeso 5:29). Huu ni ukweli unaojidhihirisha na tunajitunza wenyewe.

